# Nipashe

Jumanne Juni 23, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580265

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



Albinism Hotline

- Jifunze kuhusu Ualbino
- Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure

HAKI YETU PROJECT

Under The Same Sun

215779502




## Nafuu ya corona yarejesha huduma za Kanisa Katoliki

UKURASA 4

# Uteuzi wagombea ubunge CCM moto

**JPM** awaonya wateule wanaosaka uwaziri, asema kuongoza kura za maoni siyo kupita, aanika sababu kuwatumbua kina Gambo... *Endelea ukurasa 2*




Mhandisi Hamad Yussuf Masauni




Mohammed Aboud




Ibrahim Hussein Makungu




Ayoub Muhammed Mahmoud

# Mawaziri watatu zaidi wataka kumrithi Shein

UKURASA 3

## ACT SASA YAPULIZA KIPENGA CHA URAIS

UKURASA 3

## BAA LA CORONA



Ni muhimu kujilinda binafsi, familia na jumuiya ili kujiepusha na maambikizi ya virusi vya corona ukiwa nyumbani, sio lazima uonane na wataalamu. WHO

- **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
- **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
- **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu



MICHEZO **YANGA YAWEKA REKODI LIGI KUU** UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Magufuli awaonya wateule wanaosaka ubunge, uwaziri

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli, amewaonya viongozi ndani ya serikali wakiwamo wateule wake wanaosaka ubunge ili wateuliwe kuwa mawaziri na kuwaeleza kuwa, ni bora waridhike na nafasi walizonazo.

Alitoa onyo hilo jana Ikulu jijini Dar es Salaam wakati akiwaapisha wateule wake aliowateua mwishoni mwa wiki.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Rais Magufuli alisema kwenye siasa yanazungumzwa mengi na kutoa wito kwa viongozi anaowateua wajifunze kuridhika na nafasi walizonazo.

"Nitashangaa kama IGP (Mkuu wa Jeshi la Polisi) kama ataondoka hapa (Ikulu) aende kugombea Bunda, akagombee ubunge ategemee nitamteua kuwa waziri.

"Ningemtaka awe waziri nisingemteua tu kwenye nafasi za wabunge halafu nikamteua waziri, lakini nilimteua yeye akawe IGP wa Tanzania nzima.

"Sasa ukitoka hapa ukagombee Bunda na saa nyingine useme nitakuteua uwaziri kwanza huna uhakika kama utashinda kura za maoni na inawezekana ukashinda, lakini bado nikamfuta na hii itatokana na siku hiyo nimeamkaje."

Rais Magufuli alisema aliwahi kuteua mtu ambaye hakuwa wa kwanza, Dk. Damas Ndumbaro (Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki).

"Dk. Ndumbaro kwenye kura za maoni alikuwa mshindi wa nne, lakini wa kwanza tulimwondoa, wa pili tulimwondoa na watatu pia, na tukamchukua yeye wa nne, watu hawaelewi historia.

"Nitamshangaa CDF (Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi) ajiandae hapa aende kugombea Busega akawe mbunge akitegemea nitamteua kuwa Waziri wa Ulinzi, ndiyo maana ninasema saa nyingine ni kuridhika," alisema na kuendelea:

"Hamuwezi mkawa na kila kitu, lakini demokrasia ipo huru kama una uhakika ukienda kule utashinda tu, basi nenda kwa speed (kasi) kubwa."

Rais Magufuli aliwaeleza wenye nia hiyo kuwa kila mahali wanaweza kufanya maajabu kupitia nafasi walizonazo.

"Vinginevyo, huwezi ukawa na kila kitu, ninafahamu wewe Pima (Dk. John Pima, Mkurugenzi wa Jiji la Arusha), ulikuwa kwenye mawazo ya kwenda kumtoa Misukuma (Mbunge wa Geita Vijijini, Joseph Musukuma), nikasema ngoja nikuteue huku ili kusudi ukitaka kwenda, nenda," alisema.



Rais Dk. John Magufuli akimwapisha Idd Hassan Kimanta kuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU.**

## ...Aeleza sababu za kutumbua vigogo 3

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli ametaja sababu za kuwatumbua vigogo watatu wa mkoani Arusha, kuwa ni kitendo chao cha kila mmoja kuwa bosi kwa mwenzake na kufanya mambo binafsi badala ya aliyowaagiza.

Walioondolewa ni Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo; Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqarro na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji hilo, Dk. Maulid Madeni.

Akizungumza Ikulu jijini Dar es Salaam wakati akiwaapisha wateule hao walioteuliwa mwishoni mwa wiki kushika nafasi hizo, Rais Magufuli alisema huwa anasikitishwa anapoona aliowateua na kuwaapisha hawafanyi kazi kadri ya viapo walivyonavyo.

Wateule ni Idd Kimanta (Mkuu wa Mkoa wa Arusha), Kenan Kihongosi (Mkuu wa Wilaya ya Arusha) na John Pima (Mkurugenzi wa Jiji la Arusha).

"Mmepata majukumu mapya, nendeni mkazingatie viapo vyenu, mmeapa viapo vya maadili mkazingatie, saa nyingine huwa nasikitika sana unapoona watu uliowaapisha na kuwateua kwa kuwaamini kwa niaba ya Watanzania wanapokwenda kule hawafanyi kazi ya viapo walivyonavyo.

"Hivi karibuni ilibidi nitengue uteuzi wote Arusha niliokuwa nimewateua, kuanzia Mkuu wa Mkoa, Mkurugenzi wa Jiji na Mkuu wa Wilaya kwa sababu katika kipindi cha miaka miwili walikuwa wanagombana tu."

Rais Magufuli alibainisha kuwa kila mmoja alikuwa ni bosi na anatengeneza mizengwe kwa wenzake, kitendo ambacho hakikumfurahisha.

"Kulikuwa na mvutano wa wapi stendi ya Arusha itajengwa, mara wanang'ang'ania ikajengwe ofisi ya CCM, stendi ni ya Watanzania wote, lazima ijengwe kwenye mchepuko wa barabara," alisema.

Alisema viongozi waliopita walikuwa wanachelewesha wanaArusha kupata stendi, ndiyo maana ameamua kuwaondoa.

"Kama wanataka kubishana, wakabishane uraiani, lakini ndani ya serikali ninayoiongoza hapana, hili liwe fundisho kwa viongozi ninaowateua, ni lazima mjenge tabia za kuvumiliana.

"Kama ni kubishana na kugombana kagombane na mke wako na watoto wako, lakini ndani ya serikali hapana... ni lazima tujifunze kuzingatia sheria, maadili na viapo vyetu."

Rais Magufuli alisema walifanya kazi zao, lakini walimuudhi kwa kutoshirikiana kufanya yale aliyowaagiza.

"Nimewateua sitaki yakajitokeze, ulikuwa Mkuu wa Wilaya ya Nkasi baadaye ukaenda Monduli, na leo umekuwa Mkuu wa Mkoa.

"Bakari Msulwa ulikuwa mtangazaji Televisheni ya Taifa (TBC), umetangaza kweli, sauti nzuri tofauti na mwili wako wakati nakuteua ulikuwa ofisi ya Dodoma, umetimiza kazi yako katika utangazaji sasa tunataka ukatangaze sera za serikali.

"Kenan umekuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), ulishiriki kukimbiza Mwenge Tanzania nzima unaifahamu nchi, nimatumaini yangu Arusha haitakushinda.

Edward Barere ni Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) umefanya kazi zako Jeshi la Polisi, nina uhakika hutashindwa kwenda kufanya kazi kule Monduli.

Pima umekuwa Mkurugenzi wa Kaliua palikuwa na changamoto nyingi ukazisimamia kwa uadilifu sasa kaendelee ukasimamie uadilifu huo huo Arusha.

Jerry Mwaga umefanya kazi zako vizuri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), nina matumaini makubwa utakwenda kufanya kazi zako kule Kaliua."

Rais Magufuli aliwataka wakafanye kazi na ikiwezekana wakaridhike na walichonacho.

"Kwa sababu tatizo lingine la vijana unapowapa nafasi wana tabia ya kutoridhika na nafasi hizo, mkaridhike na nafasi mlizonazo, mkawatumikie Watanzania, nina waamini vijana, wazee wanawake, ninaamini kila mtu, kikubwa mkafanye kazi zetu mlizopangiwa," aliwasisitiza.

Alisema ni matumaini yake aliowateua watakwenda kutimiza wajibu wao na kushirikiana na viongozi watakaowakuta na kusimamia miradi mingi iliyopelekwa kwenye jiji hilo.

**AWASAMEHE WAWILI**

Katika hatua nyingine, Rais Magufuli alitangaza kuwasamehe viongozi wawili wa Jiji la Arusha ambao ni Kamanda wa Jeshi la Polisi (RPC) na Mkuu wa Takukuru, ambao wamekuwa wakifanya kazi ambazo hajawatuma.

"Leo nilikuwa niwatoe RPC pamoja na Mkuu wa Takukuru, Arusha, nimeona niwaonye hapa hapa, nimeamua kuwasamehe, lakini sijawasamehe moja kwa moja wakifanya kosa lolote wataondoka.

"Ninataka wakafanye kazi nilizowatuma siyo kazi wanazojituma wao, ninajua mtawafikishia salamu nimejitahidi sana kuwasamehe."

Alisema haiwezekani ukawa umewatuma watu wakafanye kazi za serikali wanafanya shughuli zao.

"Nyinyi mnafahamu shughuli walizokuwa wanazifanya hasa katika kipindi hiki kifupi, Mkuu wa Mkoa kawafikishie ujumbe.

"Wafanye kazi walizotumwa kulingana na mamlaka yao, wasimamie sheria, maadili yao na kwa Arusha, Mkuu wa Mkoa wewe ni jirani na Monduli unaifahamu vizuri kaisimamie migogoro ya pale."

Rais Magufuli alisema kuna migogoro mingine ilikuwa ya kutengeneza na kutolea mfano mgogoro uliokuwapo wa kanisa na shule na wa msikiti uliotaka eneo la wazi ambalo awamu tatu za uongozi zilizopita zilikataa.

"Tukijenga tabia ya ugawaji wa maeneo ya wazi hata Kanisa la Azania Front wataomba eneo la wazi lililopo Posta ya Zamani, kila mmoja ataomba maeneo ya wazi.

"Hatutakuwa na maeneo ya wazi katika miji yetu, kwa hiyo msimamo ni ule ule ambao uliwekwa na viongozi walionitangulia."

Rais Magufuli alisema tatizo lilitengenezwa na Mkuu wa Mkoa anazungumza lengo ni kuonekana ni mzuri sana.

"Kila mmoja anatoa ahadi, tusitoe ahadi ambazo hazionekani, ni lazima tusimamie sheria. Nimeyasema haya ili Mkuu wa Mkoa, Mkurugenzi na Mkuu wa Wilaya Arusha msijeingia kwenye matatizo," alisema.

Pia, alimweleza mkurugenzi huyo moja ya kazi anazotakiwa kwenda kufanya ni kuhakikisha stendi ya Arusha iliyopangwa kujengwa, inaisha.

# Mawaziri watatu zaidi wataka kumrithi Shein

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

IDADI ya makada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wanaotaka urais wa Zanzibar inazidi kuongezeka baada ya jana makada wanane wakiwamo, mawaziri watatu, kujitokeza kuchukua fomu ya kugombea nafasi hiyo.

Jana majira ya saa mbili asubuhi, aliyekuwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Rashid Ali Juma, alifika Ofisi Kuu za CCM Kisiwandui kuchukua fomu hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Rashid ambaye pia ni Mwakilishi wa Amani, alikipongeza chama chao kwa kuweka utaratibu mzuri katika uchukuaji wa fomu kwa kutoa ruhusa kwa kila mwanachama kutumia demokrasia.

"Nimefurahishwa na utaratibu wa chama katika uchukuaji wa fomu za kuwania nafasi ya urais ambao ni mfano wa kuigwa kwa vyama vingine vya siasa," alisifu.

Majira ya saa 2:58 asubuhi, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Khamis Mussa Omar, alifika katika Ofisi Kuu za CCM kuchukua fomu na kuzungumza na waandishi wa habari, akisema CCM ikimpa ridhaa ya kugombea nafasi hiyo, atailetea Zanzibar maendeleo.

Majira ya saa nne asubuhi, Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Mmanga Mjengo Mjawiri, aliwasili kwenye ofisi hizo kuchukua fomu kisha kuzuru kaburi la Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Abeid Amani Karume lililoko Kisiwandui.

Alisema amejitathmini na kuona anaweza kugombea nafasi hiyo na chama kitakapomteua, atawatumikia wananchi kwa moyo wa kujituma, uzalendo, umakini, ubunifu na utayari.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Yussuf Masauni, pia alifika Ofisi Kuu za CCM majira ya saa 10:24 asubuhi kuchukua fomu akiwa ameongozana na mke wake.

Masauni aliipongeza CCM kwa kuweka demokrasia yenye wigo mpana wa kupata viongozi na kutoa fursa kwa wanachama wake kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ikiwamo urais.

Alisema kutokana na kushika nafasi mbalimbali katika chama na serikali, ni dhahiri zimemjenga, kumwimarisha, kumkomaza na kujiamini kugombea nafasi yoyote ya uongozi wa juu ikiwamo ya urais wa Zanzibar.

Majira ya saa 4:45 asubuhi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Mohammed Aboud Mohammed, alifika Ofisi Kuu za CCM kuchukua fomu na kusema:

"Hatupo hapa kushindanisha wagombea, bali kutumia fursa tuliyopewa na chama chetu, ili kumpata mmoja wetu atakayeteuliwa na chama na kushika bendera katika kugombania nafasi ya ushindi katika uchaguzi wa hivi karibuni."

Mgombea mwingine Bakar Rashid, alifika kwenye Ofisi Kuu za CCM majira ya saa 6:15 kuchukua fomu na kusema kuwa amechukua uamuzi huo ili kuitumia haki yake kama mwanachama wa CCM ambapo kazi iliyopo mbele yake kwa sasa ni kuzisoma fomu hizo na kutafuta wadhamini.

Hussein Ibrahim Makungu, Mwakilishi wa Mtoni, alifika kwenye ofisi hizo majira ya 6:30 mchana kuchukua fomu na akakipongeza chama na kuahidi kumuunga mkono mgombea yeyote ambaye atateuliwa ikiwa yeye hatapata ridhaa hiyo.

Uchukuaji fomu kwa jana ulihitimishwa na Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, ambaye alifika kwenye ofisi hizo majira ya saa 9:39 alasiri.

Watia nia hao walikabidhiwa fomu hizo za kugombea urais na Katibu wa Oganaizesheni, Galos Nyimbo.

Wagombea 23 ambao mpaka jana walikuwa wameshachukua fomu kwa nia ya kurithi kiti kinachoachwa na Dk. Mohamed Shein ni pamoja na: Mbwana Bakari; Balozi Ali Karume; Mbwana Mwinyi Yahya; Omar Shehe; Muhammed Jafar; Muhammed Hija; Meja Jenerali Issa Suleiman Nassor; Shamsi Vuai Nahodha; Dk. Hussein Mwinyi; na Profesa Makame Mbarawa.

Wengine ni: Mwatum Mussa Sultan; Haji Rashid Pandu; Dk. Abdul-halim Mohammed Ali; Jecha Salim Jecha; Dk. Khalid Salum Muhamed; Rashid Ali Juma; Khamis Mussa; Mmanga Mjengo Mjawiri; Hamad Yussuf Masauni; Muhammed Aboud; Bakari Rashid; Ibrahim Makungu; na Ayoub Muhammed Mahmoud.



Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa na Mlezi wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam, Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan, akionyesha kadi ya chama hicho, kabla ya kumkabidhi aliyekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Vijana la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAVICHA) na Diwani wa Viti Maalum Wilaya ya Kigamboni, Stella Masanja (kulia), baada ya kukihama chama hicho na kujiunga na CCM, katika kata ya Somangile Gezaulole, jana. **PICHA: OMR**.

# ACT yapuliza kipenga urais

**Na Elizabeth Zaya**

WAGOMBEA wa nafasi ya urais wa Tanzania na Zanzibar kupitia Chama cha ACT-Wazalendo, wanatarajia kujulikana Agosti 2 mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu, alisema tayari chama hicho kimefungua milango kwa watia nia wa nafasi hiyo ya urais kuchukua fomu kuanzia Julai Mosi hadi 13 mwaka huu.

"Kamati Kuu ya Chama cha ACT-Wazalendo ilikutana kwenye kikao chake cha kawaida jijini Dar es Salaam chini ya Mwenyekiti wake, Maalim Seif Sharif Hamad. Pamoja na mambo mengine, ilipokea na kujadili kwa kina ripoti ya Sekretarieti ya Chama kuhusu maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu na kutoa maazimio," alisema.

Shaibu aliongeza: "Kamati Kuu imefungua rasmi pazia la mchakato wa uteuzi wa wagombea wa uchaguzi mkuu kwa kuchukua, kujaza na kurejesha fomu kuanzia Julai Mosi hadi Julai 13 mwaka huu.

"Julai 11 itakuwa ni kikao cha Kamati Kuu na Agosti Mosi itakuwa ni kikao cha Halmashauri Kuu na mchakato wa kuwapitisha wagombea wa pande zote mbili za muungano utahitimishwa Agosti 2 katika mkutano mkuu wa taifa.

"Hivyo basi, ninapenda kuwatangazia wanachama wote wa ACT-Wazalendo wenye nia ya kugombea kwenye nafasi za udiwani, ubunge, uwakilishi na urais wa Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakachukue fomu ifikapo tarehe hiyo."

Shaibu alisema pamoja na mambo mengine, kamati hiyo iliridhia chama hicho kufanya mazungumzo ya ushirikiano na vyama makini vya upinzani, huku ikisisitiza kulinda ushindi kwa mbinu zote.

"Kamati Kuu ya Chama imesisitiza msimamo wa chama kuwa uchaguzi mkuu wa mwaka huu utakuwa wa kufa na kupona. Chama kitahakikisha kinaulinda ushindi wake kwa mbinu zote halali na kwa gharama zozote," alisema.

Mtendaji huyo wa ACT-Wazalendo alisema Kamati Kuu pia ilisisitiza umuhimu wa chama hicho kuendelea kupinga vitendo vya rushwa.

"ACT-Wazalendo haitamvumilia mwanachama yeyote atakayejihusisha na vitendo vya rushwa kwenye uteuzi wa wagombea wake.

"Idara ya ACT-Amani imeagizwa kuchunguza na kufuatilia kwa karibu mwenendo wa mgombea wa kila nafasi na atakayebainika kushiriki vitendo hivyo, ajue fika kuwa hana nafasi ya kuteuliwa kugombea kupitia chama chetu na atachukuliwa hatua kali za kinidhamu," alisema.

Shaibu pia alisema Kamati Kuu hiyo iliwaagiza wasimamizi wa mchakato wa uchaguzi ndani ya chama hicho kwa kila ngazi kuhakikisha uteuzi wa wagombea unafanyika kwa kufuata misingi ya uhuru, haki, usawa na uwazi. mbunge Msigwa kuendelea kwenda bungeni umekwisha, sasa ajiandae kwenda kusimamia mashamba yake ya nyanya na kanisa lake kwani ubunge wa jimbo hilo ameshapoteza.

Alisema kutokana na Msigwa kujua wazi kuwa jimbo hilo si lake tena, ameamua kukimbilia kuchukua fomu ya urais Chadema, nafasi ambayo hata hivyo hawezi kuipata kwani imani ya Watanzania kwa miaka mitano ijayo ni Rais Magufuli.

Wakati huo huo, Polepole alikabidhi bajaji 10 zilizotolewa na Halmashauri ya Manispaa ya Iringa ikiwa ni sehemu ya ahadi yake aliyokuwa ameitoa kwa vijana hao kupewa mkopo nafuu wa bajaji kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Iringa.


**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

Ndugu **PAUL NGWELLE DOTTO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 141 AYW** Toyota Hiace. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa katika kituo chochote cha polisi kwa kumb: **MWA/NY/RB/467770/2020.**

115785802

**THE COMPANY ACT CAP 212 OF 2002**

**SWISSTRONICS CO.LIMITED**
**P.OBOX 70918 DAR ES SALAAM**
**COMPANY NO. 33141**

**NOTICE OF RESOLUTION TO WIND UP VOLUNTARILY**

**NOTICE:** I have given to the general public that by special resolution dated 31st January, 2020

**TAKE NOTICE:** That all the creditors are hereby requested to furnish to the chairman with full details of their claims against the Company at the Company address within 14 days from the date of this Notice.

Dated at Dar es salaam on 22nd June, 2020

**BARAKA MURASIRA MAUGO**
**Liquidator**

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
22/06/2020

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMATANO** tarehe **24/06/2020** kampuni ya **CIVIL LOTHS ENTERPRISES LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa. Kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **SONGEA** gari hilo lina namba za usajili: **T735 DRM/ T 295 DRG**

2. Magari hayo yana vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **17.80** |
| **Upana** | - | **mita** | **3.0** |
| **Kimo** | - | **mita** | **4.6** |

3. Njia itakayotumika: **DAR ES SALAAM hadi SONGEA kupitia MIKUMI** Gari litasafiri muda wa mchana tu ***(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)***

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

# Ma-RC Kanda ya Ziwa wapewa jukumu la utalii

**Na Waandishi Wetu**

KATIBU Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, amewaagiza wakuu wa mikoa ya Kanda ya Ziwa kuhamasisha wafanyabiashara wa mikoa hiyo kuwekeza kwenye sekta ya utalii.

Aidha, alisema iwapo watawekeza, itasaidia kukuza utalii kwa ukanda wa Kaskazini na Magharibi.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa Kivuko cha Kisiwa cha Rubondo na Utalii wa Sokwe wilayani Chato mkoani Geita, alisema ni jukumu la viongozi hao kwa kushirikiana na wabunge kuhamasisha kundi hilo kuwekeza kwenye sekta hiyo ikiwamo kujenga hoteli za kitalii.

"Rai kwa sekta binafsi, zipo fursa nyingi za utalii katika maeneo haya kama uwekezaji, huduma za kulala, huduma za usafiri na nyingine nyingi," alisema Balozi Kijazi.

Alisema kivuko kipya cha Mv. Rubondo Island kilichopo Kata ya Mganza wilayani humo, kimepunguza adha ya usafiri kwa watalii waliokuwa wakienda kutalii katika hifadhi hiyo, na kwamba kivuko hicho kitasaidia kukuza na kuinua uchumi wa Taifa katika sekta hiyo.

Pia, alisema kuwa kivuko hicho kimejengwa na makandarasi wa zawa wa kampuni ya Songoro Marine na umegharimu Sh. bilioni 2.3, na kwamba kina uwezo wa kubeba magari sita na abiria 50, hivyo kitaongeza pato katika sekta ya utalii.

Naye, Naibu Waziri Wa Maliasili Utalii, Costantine Kanyasu, alisema uzinduzi wa kivuko hicho ni upanuzi wa sekta ya utalii, na kwamba lengo ni kuhakikisha sekta ya utalii inakuwa katika Ukanda wa Magharibi sambamba na kuongeza pato la Taifa.

Awali, Kamishna wa Uhifadhi wa Shirika Hifadhi za Taifa (Tanapa), Dk. Allan Kijazi, alisema wamejipanga kutatua changamoto zinazowakumba watalii wa ndani na nje katika Hifadhi ya Taifa Rubondo.

"Kwa upande wa watalii wa ndani na nje kumekuwa na changamoto kubwa sana ya kufika hifadhi kama Rubondo na Saanane kwa sababu inafika mahali watalii wanatakiwa kuvuka kwenda kisiwani, lakini hakuna usafiri wa uhakika," alisema Dk. Kijazi.

**Imeandikwa na Alphonce Kabilondo, GEITA, Magdalena Haule na (UDOM).**

# Kanisa Katoliki laondoa zuio kwa shughuli zote

**Na Salome Kitomari**

KANISA Katoliki nchini limeondoa zuio la shughuli mbalimbali kutokana na janga la corona na kuanzia Jumapili ijayo zitarejea.

Kwa mujibu wa waraka uliosomwa kwenye parokia na vigango vya kanisa hilo juzi, uliruhusu kurejea kwa taratibu za ibada kama kawaida kuanzia Juni 28, mwaka huu.

Aidha, mfundisho ya Kipaimara na Komunio kwa watoto yatareja siku zijazo na waumini watatangaziwa.

Katika tangazo hilo, ibada za nyumba kwa nyumba zimerejeshwa kuanzia Jumamosi ya Juni 27, mwaka huu, lakini haitaruhusiwa kusali nyumba kwa nyumba kama awali bali waumini wasali katika eneo moja la wazi.

Aidha, katika ibada hizo wametakiwa kuzingatia umbali wa mtu na mtu, kunawa mikono kwa sabuni na muda kuwa mchache.

Pia, kanisa hilo limesema taratibu za ibada zitarejea ikiwamo kwaya kuimba kama kawaida.

Tangu kulipuka kwa ugonjwa wa corona nchini, kanisa hilo lilisitisha baadhi ya taratibu za ibada kama padri kumlisha muumini mkate, maji ya baraka ya kuweka ishara ya msalaba wakati wa kuingia na kutoka.

Kadhalika, kwaya zote zilisitishwa na muda wa ibada kufupishwa, idadi ya waumini wanaoshiriki ibada ikiwa ndogo, huku ibada zikifanyia vigangoni na parokiani pekee.

Aidha, kanisa hilo liliwataka waumini kuendelea kuchukua tahadhari ya janga la corona.

Mgonjwa wa kwanza wa corona aligundulika Machi 16, mwaka huu, na shughuli nyingi ikiwamo shule na vyuo kufungwa Machi 17, mwaka huu.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Godfrey Nyaisa (katikati), akizungumza wakati akifungua semina ya wiki moja kwa maofisa biashara wa mikoa mbalimbali kuhusu kazi za taasisi hiyo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA .**

# Shahidi adai Gugai kumwingiza mikataba ya uongo

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imeambiwa katika kesi ya kutakatisha fedha na shahidi wa 32, Manwali Masalakulangwa, kwamba Mhasibu Mkuu wa zamani wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Godfey Gugai, alikuwa anashirikiana naye mambo ya kijamiii pamoja na kumsaidia kuingia mikataba ya uongo akionyesha anamiliki viwanja vyake.

Kadhalika shahidi huyo amedai kuwa alimsaidia Gugai kuingia mikataba ya umiliki viwanja na mtu mwingine baada ya kudai kuwa amepata matatizo kazini.

Shahidi huyo alitoa ushahidi wake mwisho wa wiki iliyopita inayomkabili Gugai ikiwamo kutakatisha fedha na kumiliki mali zinazozidi kipato chake na wenzake wawili, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Masalakulangwa ambaye ni mjasiriamali mwenye digrii ya Uhusiano wa Kimataifa, alitoa ushahidi huo wa Jamhuri dhidi ya washtakiwa.

Akiongozwa na Mwendesha Mashtaka wa TAKUKURU, Ipyana Mwakatobe, shahidi alidai alifahamiana na Gugai mwaka 2009, wakiwa wanasoma chuo kimoja cha Diplomasia Kurasini, jijini Dar es Salaam kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Alidai kuwa baada ya kuhitimu masomo alishirikiana naye mambo mbalimbali ya kijamii ikiwamo misiba na harusi.

"Mheshimiwa hakimu pia tulishirikiana na mambo ya viwanja kwa sababu aliniambia kuwa ana matatizo ofisini, hivyo nimsaidie kuchukua umiliki wa viwanja visomeke kama mimi ndiye mmiliki," alidai na kuongeza.

"Pia Gugai aliniomba nimsaidie kumtafuta mtu mwingine ili aonyeshe anamiliki viwanja vyake vilivyopo mkoani Dodoma, nilikubali nilimtafutia mtu mwingine ambaye anaitwa Rose Abdallah, avichukue kama vyake na niliwakutanisha nyumbani kwangu, walisaini mikataba mitatu mwaka 2016 ya viwanja vya Gugai, lakini hatukulipa fedha na wala hatujui vilipo," alidai Masalakulangwa.

Alidai kuwa baada ya kusainiwa mikataba hiyo aliichukua na baadaye alikabidhi TAKUKURU Makao Makuu.

"Mheshimiwa Hakimu katika mikataba hiyo Gugai ni muuzaji kiwanja namba 14 block J kilichopo Bunju, Dar es Salaam kwa Sh. milioni 15 ambapo mkataba uliandikwa Novemba 15, mwaka 2015 na ploti namba 103, 104," alidai.

Shahidi huyo alidai kiwanja namba 184 block D kilichopo Temeke, Dar es Salaam, thamani yake ni Sh. milioni 10 na mikataba ya viwanja hivyo ilisainiwa siku tofauti kiwanja cha Temeke kilisainiwa mwaka 2006.

Masalakulangwa alidai tangu kusainishwa kwa mikataba hiyo hajawahi kutembelea viwanja hivyo wala kulipia fedha.

Mbali na Gugai, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni George Makaranga na Leonard Aloys.

Gugai na mwenzake, wanakabiliwa na makosa 40, kati ya hayo ni ya kughushi, utakatishaji fedha na moja ni kumiliki mali zilizozidi kipato halali.

Gugai anakabiliwa na kosa la kumiliki mali kinyume na kipato chake, anadaiwa kutenda kosa hilo kati ya Januari mwaka 2005 na Desemba mwaka 2015.

Inadaiwa mshtakiwa akiwa jijini Dar es Salaam kama mwajiriwa wa TAKUKURU alikuwa akimiliki mali zaidi ya Sh. bilioni 3.6 ambazo hazilingani na kipato chake cha awali na cha sasa, huku akishindwa kutolea maelezo.

TANGAZO


tigo rusha
Jaza kidigitali
Pata Bonus ya Dakika na Data BURE
Nunua muda wa maongezi na vifurushi kidigitali.
Haraka na rahisi kwa Tigo Rusha!
Inapatikana nchi nzima
4G+
tigo
*Vigezo na masharti kuzingatiwa
215784702

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Mapambano ya rushwa ya ngono yahusishe wote

**WAHADHIRI** wa vyuo vikuu wamepinga vikali madai ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kuwa wanashawishi rushwa ya ngono vyuoni kwa wanafunzi wa kike.

Madai hayo yalitolewa wakati kampeni maalum ya kupinga rushwa ya ngono vyuoni iliyofanyika katika Chuo cha Uhasibu (TIA) tawi la Mbeya, na kujumuisha wahadhiri wa vyuo mbalimbali.

Mmoja wa wahadhiri alitetea wenzake kwa kueleza jinsi wanafunzi wa kike wanavyochangia kasi ya rushwa ya ngono.

Alisema wanafunzi hao kuvaa mavazi ya kutega na kufanya matendo ya kuwashawishi wakati nao ni binadamu na wanaweza kuingia majaribuni.

TAKUKURU ilidai kuwa rushwa hiyo hutokea zaidi kwa ahadi ya kuwapa alama nzuri kwenye mitihani na kupanga maeneo ya kufanya mafunzo kwa vitendo na kama wahadhiri wangekuwa imara, rushwa hiyo isingekuwa inajitokeza mara kwa mara.

Tatizo la rushwa ya ngono limeonekana kuwaathiri zaidi watoto wa kike na wapo ambao hutumia nafasi zao kuwanyanyasa au kuwabania katika jambo fulani ili akubali matakwa ya wahadhiri wao.

Athari ya kuwa na rushwa ya ngono kwanza ni kunyanyasa wanafunzi kisaikolojia, kuwaumiza kimwili kwa kuwa wanashiriki tendo la ndoa kwa kupata kitu fulani (alama za ufaulu).

Nyingine ni kuambukizwa maradhi ikiwamo Ukimwi na wapo waliojikuta kwenye maisha hayo na sasa wamepoteza tumaini la maisha yao, ilhali walikwenda chuoni kwa ajili ya kusoma kwa ajili ya maisha yao ya baadaye.

Pia, athari nyingine ni kuzalisha wataalamu ambao hawajaiva kabisa kwa kuwa walifaulu si kwa kusoma na kuelewa bali kusubiri majibu ya mitihani au alama za bure, na kuonekana ni wenye vyeti vyenye ufaulu wa juu lakini kiuhalisia hawastahili.

Wapo wahadhiri wanaostahili lawama hizi kwa kuwa wamedhamiria kutenda hayo, lakini wapo ambao wamejikuta kwenye mitego ya wanafunzi wa kike na kwa matamanio ya kibinadamu wamejikuta kwenye mtego.

Baadhi ya wanafunzi wa kike hawasomi na badala yake wanajihusisha ma starehe, kutoingia darasani na hawafanyi mazoezi yanayotolewa ambayo hutengeneza alama za kumwezesha mwanafunzi kufanya mtihani wa muhula.

Mwanafunzi wa aina hii maana yake atafanya kila awezalo kuwa karibu na mwalimu wake na anapopata upenyo anaonyesha anachotaka kwa kumtega mwalimu, naye bila ya kujua anaingia kwenye mtego wa kuwa na uhusiano wa kimapenzi na kuwa na mzigo mzito wa kumbeba kimasomo katika hali isiyo ya kweli.

Baadhi ya vyuo hakuna zuio la mavazi ya kuvaa mathalani vyuo vya umma, mwanafunzi anaruhusiwa kuvaa anachoona ni sawa.

Wanafunzi wengine kwa kujua au kutojua huvaa mavazi yenye kuonyesha maumbile yao ambayo huwa ni mtego kwa wahadhiri, nao bila kujijua wanaingia kwenye mtego.

Hivyo, suala la rushwa ya ngono linapaswa kuangaliwa kwa jicho la pekee kwa kuwa wakati mwingine husababishwa na pande zote. Kutokana na tamaduni zetu ni ngumu sana kwa mwanaume kuripoti tukio la mwanaume kumtaka kwa nguvu, na wakati mwingine huona ni ufahari kutembea naye kuliko achekwe kwa kukataa vishawishi.

Pia, lipo tatizo la wahadhiri wa kike kuwataka wanafunzi wa kiume na wakati mwingine wanafunzi hushawishiwa wahadhiri, nalo si jambo la kufumbiwa macho kwa kuwa madhara yake ni makubwa. Tunaona ni vyema pande zote zikashiriki kukomesha rushwa ya ngono kwa kuhakikisha kila mmoja anatimiza wajibu wake, na inapokuwa kinyume chake hatua za kisheria zichukuliwe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Masomo yanavyoanza wanafunzi mmejipanga?

Na Sabato Kasika

**WAKATI** shule za msingi na sekondari zikitarajia kuanza masomo wiki ijayo, tayari serikali imeshatoa ratiba ya kuwezesha wanafunzi kufidia muda ambao walikaa nyumbani kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona.

Katika ratiba za masomo za kila siku, zimeongezwa saa mbili mara tu shule zitakapofunguliwa, huku walimu na wafanyakazi wakitakiwa kuzingatia maelekezo ya kujikinga na maambukizi.

Pamoja na lengo hilo zuri la serikali, ni wajibu wa wanafunzi wenyewe kutambua umuhimu wa elimu ili saa hizo mbili zilizoongezwa zisipotee na badala yake ziwe na manufaa kwao.

Nafasi hii kama wataitumia vizuri, wanaweza kusoma kwa bidii, ili kuhakikisha wanafaulu mitihani yao na kufanikiwa kwenda mbele kana kwamba hawakuwa na likizo ndefu iliyotokana na tishio la corona.

Kwa zaidi ya miezi mitatu ambayo wanafunzi walikuwa nyumbani wakisoma kwa njia ya televisheni na mitandao ya kijamii, huku wengine wakipelekewa masomo nyumbani na walimu wao.

Lakini, ujifunzaji huo ni wazi kwamba hauwezi kuwa kama ambavyo mwanafunzi anapokuwa darasani na mwalimu wake, hivyo kuongeza muda wa saa mbili kunakusudia kuwaweka wanafunzi sawa zaidi.

Kwa hiyo kama ambavyo Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alitangaza ratiba za mitihani ya taifa darasa la saba, kidato cha nne na upimaji wa kitaifa wa darasa la nne na kidato cha pili.

Hivyo utaratibu huo uliotangazwa na serikali ni wa muhimu iwapo utazingatiwa ili kuhakikisha wanafunzi wanafaidika na masomo, hasa wale wanaojiandaa kufanya mitihani ya taifa.

Lakini, anasisitiza kuzingatia maelekezo ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kwa kuhakikisha shule zinanunua vifaa vya kutosha kwa ajili ya kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni.

Waziri anatoa ratiba hiyo baada ya Rais John Magufuli, kuagiza shule zote za msingi na sekondari kufunguliwa Jumatatu Juni 29, na kuruhusu shughuli nyingine za kijamii zilizokuwa zimezuiwa kuendelea kama kawaida.

Kwamba wanafunzi watalazimika kusoma saa mbili zaidi katika ratiba za masomo, angalau kufidia muda ambao walikaa nyumbani wakati wa sakata la kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona.

Hivyo hiyo ni nafasi nzuri kwa wanafunzi kuchangamkia hizo saa mbili zilizoongezwa katika ratiba za masomo ili kujiandaa vizuri kwa ajili ya mitihani ya taifa ambayo iko mbele yao.

Saa hizo zimeongezwa kwa kusudi maalum hivyo ni vyema wanafunzi wakazingatia ratiba hiyo ili mwisho wa siku iwanufaishe, kwa kuwa ni muhimu wawe na maandalizi ya kutosha kabla ya mitihani.

Ratiba iko wazi kwamba shule za msingi na sekondari wanafunzi watarejea shuleni Juni 29, mwaka huu na kumaliza muhula wa kwanza wa masomo Agosti 28, na kuanza muhula wa pili ambao utaisha Desemba 18.

Kwa mujibu wa wizara husika, ratiba ya mitihani ya darasa la saba itaanza Oktoba 7 hadi Oktoba 8 mwaka huu, huku kidato cha pili ikianza Novemba 9 hadi Novemba 20 mwaka huu.

Nao kidato cha nne wanatarajia kuanza mitihani Novemba 23 hadi Desemba 11 mwaka huu na darasa la nne wataanza Oktoba 25 hadi Oktoba 26 mwaka huu, hivyo umuhimu wa saa mbili za ziada upo palepale.

Hii inatokana na ukweli kwamba, ili kukamilisha muhtasari wa masomo, shule zitalazimika kuongeza saa mbili za masomo kwa ajili ya kufidia muda uliopotea kama ambavyo Prof. Ndalichako anasema.

Ni wajibu wa wanafunzi kuzingatia ratiba hiyo ili iwe na manufaa kwao, kwani baadhi yao huwa wana kawaida ya kukwepa vipindi vya masomo ni wepesi wa kujificha wakikwepa masomo na kwenda kucheza.

Wanafunzi wa aina hiyo wadhibitiwe na inawezekana ndiyo hao ambao hata wakati wa likizo walikuwa hawafuatilii masomo kupitia televisheni, redio au mitandao ya kijamii, hivyo wasaidiwe kuachana na mtindo huo.

Kuzingatia ratiba ya masomo kunaweza kusaidia kuboreshwa na hasa wakati huu ambao Tanzania inajipanga kufikia uchumi wa viwanda 2025, kwa kuandaa wataalamu wa baadaye.

# Benki ya Exim yahamasisha huduma za kidigitali

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Exim imezindua kampeni yake mpya inayolenga kuhamasisha wateja wake kutumia zaidi huduma za kidigitali ili kurahisha upatikanaji wa huduma zinazotolewa na benki hiyo.

Pia, lengo la lampeni hiyo 'Maliza Kirahisi Kidigitali' ni kuokoa muda ambao wangeutumia kufuata huduma hizo kwenye matawi ya benki hiyo.

Kampeni hiyo imekuja kipindi ambacho jamii inapitia mabadiliko kuelekea huduma za kidigitali hususani katika huduma za kifedha na manunuzi, hali iliyochochewa zaidi na mlipuko wa ugonjwa wa virus vya Corona (COVID 19).

Benki hiyo imesema kampeni 'Maliza Kirahisi Kidigitali' itadumu katika kipindi chote cha mwaka kilichobaki, na kwamba itahamasisha wateja wa benki kufanya mihamala ya kibenki muda wowote na mahali popote kwa kutumia simu zao pamoja na njia za kimtandao.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo jijini Dar es Salaam hivi karibuni, Mkuu wa Huduma ya Rejareja wa benki ya Exim, Andrew Lyimo, alisema: "Kampeni ya 'Maliza Kirahisi Kidigitali' inakusudia kubadilisha tabia ya watumiaji wa huduma zetu yaani wateja wetu na zaidi pia inalenga kuongeza kasi ya mabadiliko ya nchi kutoka kwenye kufanya mihamala ya pesa kwenda kwenye mihamala ya kidijitali hususani wakati wa janga hili la Corona."

"Hivyo basi kampeni hii imekuja wakati mwafaka kwa maana ya kipindi ambacho taifa linaelekea kwenye mabadiliko ya kihuduma za kifedha ili kuepuka misongamano ya watu kwasababu za kiafya na wakati huo huo tukirahisisha utoaji wa huduma zetu wateja pamoja na kuongeza usalama wa fedha zao," alisema.

Lyimo alisisitiza: "Ili kufanya huduma za kibenki ziwe nzuri zaidi na rahisi kwa wateja, Exim benki tunazo chaguzi kadhaa ikiwemo kutumia huduma ya mobile bank inayohusisha matumizi ya simu za mkononi au kwa njia ya USSD, kutumia kadi zetu za benki, mtandao wetu wa POS na pia kutumia huduma za mtandaoni kupitia wavuti au programu (App) ambazo zinawawezesha wateja wetu kupata huduma muhimu za kifedha muda wote."

Alisema kupitia huduma hizi wateja wanaweza kufikia akaunti zao, kuangalia salio au kufanya miamala ya kibenki kwa njia ya mtandao wakiwa majumbani mwao, vyuoni, ofisini, sehemu za biashara au mahali popote, hivyo kuokoa muda wao ili wautumie kutimiza majukumu yao mengine.

Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano wa benki hiyo, Stanley Kafu, alisema kampeni hiyo imekuja mwaka mmoja tangu benki hiyo izindue kampeni maalum iliyolenga kuhamasisha wateja wake kuhusiana na matumizi ya mtiririko wa huduma maalumu za kiusalama kwenye masuala ya fedha zinazotolewa na benki hiyo.




Mkuu wa Huduma ya Rejareja wa Benki ya Exim, Andrew Lyimo (katikati), akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani), wakati wa uzinduzi wa kampeni mpya ya benki hiyo ijulikanayo 'Maliza Kirahisi Kidigitali' inayolenga kuhamasisha wateja wa benki hiyo kutumia zaidi huduma za kidigitali. Wengine ni Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano wa benki hiyo, Stanley Kafu (kushoto) na Mkuu wa Idara ya Kidigitali na Huduma Mbadala, Silas Matoi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# Ashtakiwa kutakatisha Dola za Marekani 898,000

**Na Hellen Mwango**

MFANYABIASHARA Salum Rajabu (51), mkazi wa Maili Moja Kibaha, mkoani Pwani, amefikishwa mahakamani akikabiliwa na mashtaka mawili ikiwamo kujipatia fedha na kutakatisha Dola za Marekani 898,000.

Mshtakiwa huyo alisomewa mashtaka yake jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashidi Chaungu.

Wakili wa Serikali Esther Martin, alidai kuwa katika shtaka la kwanza kati ya Aprili 1 na 20, mwaka huu, jijini Dar es Salaam, Mvomero mkoani Morogoro, na Lubumbashi nchini Congo, mshtakiwa akiwa raia wa Tanzania alijipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa alijipatia Dola za Marekani kutoka kwa Segere Bushiri, Rocky Kungala na Paty Lufumada Dola za Marekani 898,000, baada ya kutakiwa kuziwasilisha nchini Tanzania kwa Albert Makendi Mayombo.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa tarehe na mahali pa tukio la kwanza, mshtakiwa alitakatisha Dola za Marekani 898,000 wakati akijua ni zao la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Mshtakiwa hakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi.

Martin alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na kuiomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu Chaungu alisema kesi hiyo itatajwa Julai 6, mwaka huu na mshtakiwa apelekwe mahabusu.

# Waziri abaini tatizo machimbo Kisarawe

**Na Mwandishi Wetu,** KISARAWE

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, amezuru katika eneo la machimbo ya madini ya kaolin yanayomilikiwa na Kampuni ya Rakkadlin Co. Ltd wilayani Kisarawe na kubaini tatizo la kimazingira ikiwamo kampuni kutokuwa na cheti cha tathmini ya athari kwa mazingira.

Katika ziara yake hiyo, Zungu alifuatana na Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo, Meneja wa Kanda ya Mashariki wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Anorld Mapinduzi, wanasheria kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, NEMC pamoja na viongozi mbalimbali wilayani Kisarawe.

Viongozi hao walijionea shughuli za uchimbaji wa madini hayo yanayotumika kutengeneza malighafi za marumaru.

"Tumepitia matamko ya mwekezaji na ya wataalamu wetu na tumeona tatizo lipo. Mwekezaji alipewa masharti toka mwaka 2018 arekebishe, lakini mpaka leo bado hajayarekebisha. Biashara inaendelea na malalamiko ya wananchi bado yapo.

"Kwa hiyo, Mheshhimiwa DC (Mkuu wa Wilaya), tutakupa matokeo ya 'findings' zetu kwa mwanasheria wa NEMC na wa Ofisi ya Rais ni hatua zipi ambazo tutazichukua," Zungu alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Mwegelo, alisema wamilikiwa wa eneo hilo wanaonekana kutokujali kabisa juu ya utaratibu uliopo na kuwataka kuheshimu sheria.

"Hapa inavyoonekana kuna uholela, vitu havijakaa sawa. Na Mheshimiwa Waziri, ninadhani na wewe umejionea. Siyo kwamba hatuhitaji wawekezaji, siyo kwamba Kisarawe haina mali, lakini muhimu sheria na taratibu zifuatwe. Hayo yote yakifuatwa, hata wananchi watakuwa wanafurahia mradi," alisema.

Meneja wa NEMC Kanda ya Mashariki, Mapinduzi, alisema kuwa mwekezaji anayehusika na mradi huo, anatakiwa kufuata utaratibu wa kimazingira, ili kuepusha madhara zaidi.

"Anavyoelekezwa kuzingatia yale matakwa ya kimazingira kuendana na sheria na kanuni ni kwa faida yake. Wananchi wakiathirika, hataweza kulipa hayo maisha ya wananchi.

"Wananchi wakitoka na kuja kumharibia kutokana na kushindwa kuridhika kutokana na vitendo anavyoyowafanyia, itakuwa ni hasara kwake. Kwa hiyo, ni vizuri anavyoyopewa maelekezo akayatekeleza kwa wakati," alisema.

Mmiliki wa Machimbo hayo, Adam Iremu, alisema kuwa anasubiri mwafaka wa mgogoro huo atakapoitwa na Waziri kama alivyoeleza.

"Kikubwa ni wakishaniita, nitakwenda na mimi nitoe ushahidi wangu na vielelezo vyangu na ndiyo nitafahamu uamuzi watakaoutoa," alisema Iremu.

# Bashiru ataja ukomo ubunge, udiwani CCM

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi(CCM), Dk. Bashiru Ally, amewataka wabunge, wawakilishi na madiwani wa chama hicho kuendelea kutekeleza ahadi zao kwa wananchi hadi dirisha la uchukuaji fomu za kugombea litakapofunguliwa mwezi ujao.

Kwa kuzingatia ratiba hiyo, amewataka makatibu wa mikoa wa chama hicho kuacha kufukuzana nao kwa madai kuwa wanafanya kinyume cha kanuni kwa kuwa bado wako kazini.

Kauli hiyo aliitoa juzi alipoongoza kikao cha mafunzo kwa makatibu hao na watumishi wa makao makuu na kulazimika kutoa ufafanuzi wa ukomo wa ubunge, uwakilishi na udiwani kupitia CCM.

Alisema kwa mujibu wa katiba na taratibu za CCM, watatekeleza ahadi kwa wananchi hadi dirisha la uchukuaji wa fomu za kugombea linapofunguliwa Julai 14 mwaka huu.

"Mbunge ama mwakilishi anayehangaika siku mbili ama wiki mbili kabla ya uchaguzi, mnahangaika naye wa nini? Kama amedondoka, atakusingizia wewe katibu, alinizuia nisikutane na wananchi kumalizia ahadi zangu, kumbe alishajifia miaka minne iliyopita, unahangaika naye wa nini," alisema.

Katibu huyo alisisitiza viongozi hao waachwe waendelee kutekeleza majukumu yao kikatiba ikiwa ni pamoja na kuwa wajumbe wa vikao mbalimbali.

"Hoja ya wabunge, wawakilishi na madiwani kuendelea ama kutoendelea na kazi ni kuwa wote hao bado wapo kazini, ukitaka mbunge asiwe kazini, maana yake Waziri Mkuu, Spika wa Bunge wote wasiwe kazini kwa sababu wote ni wabunge.

"Hatuwezi tukaacha ombwe la uongozi, nchi itaendeshwaje? Kwa sababu ya uchaguzi? Chama hiki siyo cha uchaguzi, ni chama cha uongozi," alisema.

Dk. Bashiru alisema kanuni hazijawafuta kazi viongozi hao kwa kuwa bado wako kazini na wanapaswa kutekeleza majukumu yao.

"Ninasikia mnafukuzana huko kama digidigi na wabunge na madiwani eti kwa sababu ya kanuni, kanuni hazijawafuta kazi, wale ni wajumbe wa vikao vyote vya kazi na ni wawakilishi wetu, wanatakiwa kufanya kazi ya chama na kazi ya umma mpaka tarehe 14 Julai 2020 wanapochukua fomu," alisema.

Akizungumzia mafunzo hayo, Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Abdulla Sadaalla, alisema kwa kuwa wanaingia katika uchaguzi wa dola, wameona umuhimu kukutana na makatibu hao maana ndiyo wasimamizi wa uchaguzi ngazi ya chama.

"Tumeona ni muhimu kukutana nao kwa kuwa wao ndiyo watakaosimamia uchaguzi na watapaswa kushuka chini kuanzia ngazi ya wilaya, majimbo mpaka kata," alisema.



Naibu Waziri wa Ujenzi, Elias Kwandikwa (kushoto), akizungumza na Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Christopher Ole Sendeka, wakati akikagua ujenzi wa barabara ya Njombe - Moronga - Makete yenye urefu wa km 107.4 kwa kiwango cha lami, mkoani humo, juzi. **PICHA: WUUM**

# Polisi yashikilia wawili madai kuhujumu mradi Ziwa Victoria

**Na Welingtone Masele,** TABORA

JESHI la Polisi mkoani Tabora limewatia mbaroni watu wawili kwa tuhuma za kuhujumu miradi ya maji ukiwamo wa Ziwa Victoria kwenda mkoani humo katika operesheni iliyofanywa na jeshi hilo.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari, Kamanda wa Polisi Mkoani wa Tabora, Barnabas Mwakalukwa, alitaja waliokamatwa kuwa ni Creti Mabula (20), mkazi wa mtaa wa elimu wilayani Igunga na wenzake wanne.

Alisema Mabula na wenzake walikamatwa wakiwa na mali za wizi zinazokadiriwa kuwa na thamani ya Sh. milioni 57.6.

Alifafanua kuwa vifaa hivyo vyote vinamilikiwa na Kampuni ya Wachina ya Afcons-SMC JVC REF inayotekeleza mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Tabora unaofadhiliwa na serikali kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 600.

Vile vile, Kamanda alisema kuwa Jeshi la Polisi limemkamata Thomas Katoro (38), mkazi wa Nzega na wenzake watatu kwa kukutwa na pampu kubwa ya kuvuta maji mali ya halmashauri ya wilaya hiyo yenye thamani ya Sh. milioni 32.

Alisema baada ya kuhojiwa na polisi, watuhumiwa walikiri kuiba pampu hiyo na kwenda kuiuza mkoani Shinyanga huku wakieleza kuwa waliifungua kutoka kwenye mradi ilipokuwa imefungwa.

Pia, alisema watuhumiwa hao tayari wamefikishwa mahakamani na kufunguliwa kesi ya uhujumu uchumi wa miundombinu ya miradi ya maendeleo.

Alionya vitendo vya wizi au uhalifu wa namna yoyote wa mali ya umma ikiwamo miundombinu ya miradi ya maendeleo havitafumbiwa macho na kwamba Jeshi la Polisi limejipanga vizuri na yeyote atakayebainika atashughulikiwa.

Kadhalika katika tukio lingine jeshi hilo limemkamata Ramadhan Juma (65), mkazi wa Ndekeli, wilaya ya Nzega akiwa na silaha aina ya shotgun yenye namba za usajili TZCRA 36462 na risasi nne za shotgun, alizohifadhi ndani ya nyumba yake.

Kamanda Mwakalukwa alisema mtuhumiwa huyo alikuwa akiiazimisha kwa wahalifu ambao walikuwa wakiitumia katika matukio mbalimbali ya kihalifu likiwamo la unyang'anyi wa kutumia silaha lililotokea katika kijiji hicho.

## Wanawake waaswa matumizi mabaya ya simu za mkononi

**Na Beatrice Moses**

WANAWAKE wanaotumia vibaya simu za mkononi, ikiwamo kusambaza picha zao za utupu, wameshauriwa kuona umuhimu wa kuzitumia kusaka fursa za kiuchumi ili kujikomboa katika umasikini.

Mkurugenzi Mtendaji Zaina Foundation, Zaitun Njovu, aliyasema hayo juzi kwenye mafunzo maalum ya kuwajengea uwezo wanahabari katika matumizi ya teknolojia ya mawasiliano.

Alibainisha kuwa wanawake kadhaa wamejikuta mikononi mwa vyombo vya sheria kutokana na matumizi mabaya ya simu zao za mkononi.

"Wapo wanaojipiga picha za utupu, wengine wasambaza kwenye mitandao, wengine wanatumia lugha chafu, ni vyema wabadilike."

Katika mafunzo hayo yaliyofanyika jijini Dar es Salaam, Zaitun alisema kuna fursa nyingi za kiuchumi na elimu kwenye mitandao ya kijamii ambapo zikitumiwa vyema zinaweza kusaidia kuinua jamii na kusonga kimaendeleo.

Alisema wameamua kutoa elimu kwa wanahabari kwa kuwa ni miongoni mwa watu wanaoweza kuingia kwenye matatizo kutokana na sheria, lakini wapo kwenye hatari ya mawasiliano yao kudukuliwa, hivyo kuwa shakani kiusalama.

"Mbaya ni kwamba watumiaji wengi pia hawajui kuna wadukuzi wa mawasiliano, pia sheria za matumizi ya simu hasa hizi za kisasa, mfano line (namba) tunazotumia licha ya kwamba unasajili kwa jina lako, lakini siyo mali yako, ni mali ya kampuni ya simu," alisema na kuongeza:

"Pia tunaruhusu kuchunguzwa kwa namna moja ama nyingine kulingana na matumizi ya mitandao ya kijamii."

Alisema kwa kutambua umuhimu wa elimu ya matumizi sahihi, Zaina Foundation imeamua kujikita katika kuwaelimisha wanawake na watoto wa kike na wanaume wachache ili kuwawezesha juu ya matumizi sahihi ya mitandao na mifumo ya kidijitali pamoja na jinsi ya kujikinga na unyanyasaji wa kijinsia.

" Mafunzo yanalenga pia kuwezesha wasichana na wanawake katika kujenga uwezo wa faragha na mafunzo, kuendeleza na kusaidia wanawake ambao ni waandishi wa habari, watetezi wa haki za binadamu, wanafunzi wa teknolojia, wanasheria, na kuboresha kabisa njia pamoja na kujilinda na taarifa za kwenye mitandao," alisema Zaituni ambaye ni mtaalamu wa teknolojia za habari na mawasiliano.

Mwenyekiti wa mafunzo hayo Prince Samatta, aliwasihi wanahabari kuzingatia mafunzo waliyopewa ambayo yanalenga pia kuwasaidia kuwasiliana katika hali ya usalama ili kuepuka hatari za mitandaoni na kuingia kwenye migogoro na mamlaka zinazohusika.

# Maofisa biashara watakiwa kushawishi uanzishaji viwanda

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imewataka maofisa biashara nchini kuwashawishi wananchi kuanzisha biashara na kujenga viwanda vidogo na vikubwa.

Maagizo hayo yalitolewa jana jijini Dar es Salaam na Ofisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Godrey Nyaisa, wakati akifungua mafunzo ya wiki moja kwa maofisa biashara wa mikoa ya Mbeya, Mwanza na Mtwara.

Alisema BRELA inawajengea uwezo maofisa biashara wa mikoa mbalimbali nchini ili waweze kufanyakazi zilizokuwa zinafanywa na maofisa wa BRELA mikoani lengo ikiwa ni kupunguza gharama za uendeshaji.

Alisema maofisa biashara wanatakiwa kujenga urafiki na wananchi ili iwe rahisi kufanyakazi kwa pamoja na kwa ushirikiano tofauti na ilivyokuwa zamani ambapo maofisa hao walikuwa wanaogopwa.

"Zamani maofisa biashara mliogopeka sana kiasi kwamba watu wengine walikuwa wakiwaona wanafunga maduka mpaka mpite, lakini sasa inabidi tubadili mtazamo huo tuwe marafiki na tufanye kazi kwa ushirikiano," alisema Nyaisa.

Nyaisa alisema maofisa hao mbali na kuwahamasisha wananchi kuanzisha biashara, pia wanatakiwa kuwatafutia masoko ya bidhaa zao ili kuwahamasisha wengine kuanzisha biashara na wengine kujenga viwanda.

Alitaja mafunzo watakayopata maofisa hao ni jinsi ya kusajili jina la biashara, kuhuisha taarifa za kampuni, jinsi ya kusajili leseni ya kiwanda, kuomba leseni za biashara kundi A na B na kusajili nembo za biashara.

Nyaisa alisema mwaka huu mpya wa fedha BRELA itazigawa kanda mbalimbali ambapo maofisa wake wataenda kufundisha maofisa biashara namna ya kutumia mifumo ya BRELA kusajili biashara na kazi zingine.

Alisema BRELA pia imewapatia vifaa vya TEHAMA baadhi ya halmashauri kama Ilala jijini Dar es Salaam, Chalinze mkoani Pwani na Mwanza ili waweze kusajili wafanyabiashara kidijiti.

Kwa mujibu wa mtendaji huyo mkuu, wataendelea kuzipatia halmashauri zingine vifaa vya TEHAMA ili kurahisisha upatikanaji wa leseni na hatimaye kuongeza mapato ya serikali.

# Mikoa mitatu kuunganishwa kwa lami

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema iko katika hatua za mwisho kuunganisha mikoa ya Morogoro, Njombe na Ruvuma kwa barabara za lami ili kufungua sekta ya usafirishaji katika mikoa hiyo inayozalisha mazao na misitu.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Ujenzi, Elias Kwandikwa, wakati akizungumza na wakazi wa Kisegesa Halmashauri ya Mlimba, Wilaya ya Kilombero, mkoani Morogoro, baada ya kukagua eneo lililokarabatiwa na Wakala wa Barabara (TANROADS).

Naibu Waziri huyo alikagua eneo hilo ambalo liliathiriwa na mvua na kukata mawasiliano kati ya Mlimba na Ifakara na kusababisha usumbufu kwa wasafirishaji.

"Niwatoe hofu wananchi wa maeneo haya na maeneo jirani kuwa serikali yenu imejipanga kikamilifu kuhakikisha inapandisha uchumi wa mwananchi na Taifa hili kwa kuwaunganisha na barabara za lami siku zijazo," alisema.

Aidha, aliwahakikishia wananchi wa Kilombero na Mlimba kuwa serikali itafanya marekebisho makubwa katika barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 220 kutoka Ifakara hadi Madeke.

Alibainisha kuwa kazi zinazoendelea ni usanifu kwa ajili ya kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

"Hizi hatua zinazoendelea za kukarabati ni kuhakikisha wananchi kwanza wanapita bila ya kupata usumbufu wowote, lakini lengo la serikali ni kuwaunganisha wananchi hawa kwa barabara za lami," alifafanua Naibu Waziri huyo.

Kwandikwa alielezea miradi ya ujenzi inayoendelea katika ukanda huo ikiwamo ya barabara ya kutoka Ifakara kuelekea Mikumi ambayo mkandarasi yupo eneo la mradi anaendelea na kazi na serikali iko katika mpango wa kuunganisha mkoa wa Morogoro na Iringa kupitia Mlimba hadi Kilolo kwa barabara ya lami.

Kwa mujibu wa waziri huyo, katika kuunganisha mkoa wa Morogoro na Ruvuma, serikali imeshaifungua barabara hiyo kwa kuanza kuifanyia usanifu kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kuanzia Lupilo kupitia Kilosa kwa mpepo hadi Namtumbo.

Katika hatua nyingine, Naibu Waziri huyo ameielekeza TANROADS nchini kukarabati maeneo yote yaliyoathirika na mvua na kukata mawasiliano kulingana na asili ya maeneo hayo kwa suluhisho la kudumu.

Awali, Mkuu wa Kitengo cha Uhandisi wa TANROADS, mkoa wa Morogoro, Mhandisi Baraka Mwambage, alisema wamefungua mawasiliano katika barabara hiyo kwa kuchukua hatua ya dharura, na kwamba suluhisho la kudumu linakuja kwa kuanza sasa ujenzi wa maboksi kalvati yenye midomo mitatu itakayoweza kuhimili maji mengi katika eneo hilo.




Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene (katikati), akizungumza na wajumbe wa Bodi ya Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi, jijini Dar es Salaam juzi. Wa pili kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Prof. Suffian Bukurura na (kushoto) ni Katibu wa Bodi, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), John Massawe. **PICHA: WMNN**

# RC aagiza kurudishwa M/Kata kujibu tuhuma

**Na Tiganya Vincent**, TABORA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, ameagiza kurudishwa kwa Mtendaji wa Kata aliyehamia Ilolangulu kutoka kituo chake cha zamani cha Igalula wilayani Uyui ili kujibu tuhuma dhidi yake.

Mtendaji huyo anakabiliwa na tuhuma za kukusanya fedha kwa waganga wa jadi na tiba mbadala bila kuwapatia stakabadhi.

Alisema mtuhumiwa huyo, Said Mabuga, ametuhumiwa kukusanya mapato mbalimbali na kuandika katika karatasi ya daftari bila ya kutoa stakabadhi halali, ambayo zingeonyesha uhalali wa malipo anayokusanya.

Mwanri alitoa kauli hiyo jana akiwa katika Kata ya Igalula wilayani Uyui wakati wa kuhamasisha wafanyabiashara wadogo kuchukua vitambulisho ili waweze kufanyakazi zao kwa amani.

"Tunataka aandikiwe barua ya kurudi hapa ili aje kujibu tuhumu zilizoelezwa na wananchi hapa ambazo ni kukusanya fedha za wananchi bila ya kuwapa risiti...tunataka kujua anakusanya kwa utaratibu upi na zinakwenda wapi," alisisitiza Mwanri.

Alisema TAKUKURU wilayani humo inapaswa ifanyie uchunguzi tuhuma hizo na kama kuna fedha zimechukuliwa kinyume cha utaratibu kwa wananchi zirejeshwe na mtuhumiwa achukuliwe hatua zaidi.

Mganga wa jadi, Miraji Adam, alisema kwa maelezo yaliyotolewa, nao watatakiwa kuchukua kitambulisho cha wajasiriamali wadogo kwa gharama za shilingi 20,000, lakini pamoja na kufanya hivyo watendaji wamekuwa wakiwatoza gharama nyingine.

Adam alisema gharama ambazo wamekuwa wakitozwa zinafika shilingi 105,000 ili kupata kibali ya kuendesha shughuli zao.

Alisema wanatakiwa kulipa shilingi 10,000 za Mtendaji wa Kijiji, shilingi 10,000 za Mtendaji wa Kata kusaini barua ya kuomba leseni, gharama za leseni shilingi 35,000 na shilingi 50,000 ada ya halmashauri kwa ajili ya Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala.

Adam alisema fedha hizo zimekuwa nyingi na kipato chao bado ni kidogo kama walivyowafanyabiashara wengine.

Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Thomas Masese, alisema waganga wa jadi kama walivyo wafanyabiashara wadogo, wanatakiwa kupata kitambulisho hicho ambacho gharama yake ni shilingi 20,000.

# Wahamiaji haramu 18 watiwa mbaroni

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

IDARA ya Uhamiaji mkoani Mwanza, imekamata wahamiaji haramu 18 wilayani Magu kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Juni mwaka jana hadi Juni mwaka huu.

Kamishna Msaidizi wa Uhamiaji, Bahati Mwaifuge, ambaye ni Ofisa Uhamiaji mkoani Mwanza, alisema jana kuwa kati yao, wawili wanatumikia kifungo, tisa walirudishwa kwao na watatu walipewa muda wa kurekebisha hadhi za kiuhamiaji.

"Idara yetu wilayani Magu tangu ianzishwe, tumewakamata wahamiaji haramu 18, kati ya hao, tisa tuliwarudisha kwao, wawili wanatumikia kifungo na watatu tuliwapa muda wa kurekebisha hadhi za kiuhamiaji," alibainisha.

Mwaifuge alisema lengo la kuanzishwa kwa Ofisi ya Uhamiaji katika wilaya hiyo ni kuongeza huduma karibu na wananchi, kuongeza udhibiti wa uhamiaji haramu, kuongeza ulinzi na usalama kwa kushirikiana na vyombo vya dola, kama vile Polisi, Magereza, Takukuru na vyombo vingine vya serikali.

Alisema raia wa kigeni anatakiwa kuja nchini akiwa na hati ya kusafiria na akifika, lazima Alisema raia wengi waliokamatwa ni kutoka nchi jirani za Kenya, Burundi, Uganda, Ethiopia na India, mmoja wao akiwa ni mwanamke kutoka Kenya.

Mwaifuge alikumbusha kuwa mhamiaji haramu ni mtu anayeingia nchini kwa njia za panya, na anayeingia kihalali nchini kwa kufuata sheria za uhamiaji, lakini baada ya kuisha muda wake akaendelea kuishi nchini kinyume cha sheria.

Alisema idara hiyo imekuwa ikitoa elimu kwa viongozi na jamii katika ngazi za vijiji na kata wilayani humo juu ya kutambua wahamiaji haramu na kutoa taarifa kwenye ofisi zake.

Alitoa wito kwa wananchi kuendelea kushirikiana na Idara ya Uhamiaji, ili kuwafichua wahamiaji haramu katika wilaya hiyo na kwamba kampuni, taasisi na mashirika mengine ya umma, viwanda wenye wageni ni vyema kufika katika idara hiyo ili kupata huduma stahiki.



Mafundi wakibadilisha nguzo za umeme ili kupisha ujenzi unaoendelea wa barabara ya Shekilango, katika eneo la Sinza Kijiweni, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Wana-CCM 2,565 wilayani Ruangwa wamdhamini JPM

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameongoza wanachama 314 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani Ruangwa, mkoani Lindi katika kujaza fomu za kumdhamini Rais John Magufuli ili aweze kuteuliwa kugombea tena nafasi ya urais.

Idadi hiyo inafanya jumla ya wanachama waliojitokeza kumdhamini Rais Magufuli katika wilaya hiyo kufikia 2,565, baada ya wanachama wengine 2,251 kujaza fomu hizo Jumamosi na kumdhamini.

Waziri Mkuu aliwaongoza wanachama hao juzi katika ofisi za CCM wilayani Ruangwa. Aliwasihi wananchi hao waendelee kuwa na imani na Rais Magufuli pamoja na serikali anayoiongoza.

"Mheshimiwa Rais Dk. John Magufuli ametekeleza ahadi zote alizoziahidi ikiwamo ya kuwatumikia Watanzania wote hasa wanyonge. Amewatumikia Watanzania wote bila ya kujali itikadi zao za kisiasa na hata za kidini. Nawapongeza wana CCM wenzangu mliojitokeza kumdhamini rais wetu."

Waziri Mkuu aliongeza: "Kitendo mlichokifanya kinaonyesha shukrani kubwa kwa Mheshimiwa Rais Magufuli ambaye wakati wote ameonyesha mapenzi makubwa kwetu pamoja na Watanzania wote kwa ujumla."

Alisema kwa sasa Wilaya ya Ruangwa imepata mabadiliko makubwa kimaendeleo ambayo awali hayakuwapo kama nishati ya umeme, maji ambayo kwa sasa kila kijiji kina kisima, shule za msingi katika kila kijiji na sekondari kwenye kata zote pamoja na barabara za lami katika mitaa ya mji wa Ruangwa. Haya yote ni Dk. Magufuli."

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Lindi, Fadhili Juma, alisema wanaCCM wa mkoa huo wapo bega kwa bega na Rais Magufuli, na kwamba watahakikisha anapata kura nyingi katika uchaguzi ujao.

Awali, Waziri Mkuu aliwashukuru wanaRuangwa wote kwa ushirikiano waliompatia katika kipindi chote cha miaka mitano ambao walimwezesha kutekeleza majukumu yake ya kuwaletea maendeleo kwa ufanisi mkubwa.

# Mgogoro wafanyakazi daraja Mto Kilombero wamalizwa

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imetatua mgogoro wa wafanyakazi waliokuwa wanafanya kazi ya ujenzi katika Daraja la Mto Kilombero kwenye kampuni ya kikandarasi ya China Railway 15 Group uliodumu kwa zaidi ya miaka minne na kuhakikisha haki inatendeka kwa kila mfanyakazi.

Mgogoro huo uliosimamiwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Elius Mwakalinga, pamoja na wataalamu kutoka sekta hiyo kwa muda wa siku tatu.

Aidha, imeagiza uongozi wa kampuni hiyo kuwalipa wafanyakazi hao 109 kati ya 269 waliohakikiwa na kuelekeza wafanyakazi 160 waliobaki uhakiki wao ufanyike kwa haraka ili waweze kulipwa stahiki zao.

Akizungumza na wafanyakazi hao, Naibu Waziri wa Ujenzi, Elias Kwandikwa, alisema serikali iko kwa ajili ya kuhudumia wananchi, huku akiwashukuru wafanyakazi hao.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo, kila mtu atalipwa anachostahili kwa kuwa mkandarasi amekubali kulipa mpaka mtu wa mwisho.

Aidha, Kwandikwa aliishukuru ofisi ya mkuu wa wilaya na ofisi ya kazi mkoa, kwa ushirikiano wao katika kuhakikisha wananchi hawa wanapata haki zao.

Mmoja wa wafanyakazi hao, Ramadhani Selemani, alisema amelipwa fedha alizokuwa anadai na kuishukuru serikali kwa kusimamia haki yao kupatikana.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa wafanyakazi wa ujenzi wa daraja la Mto Kilombero , Alex Ndagaro, alisema mwaka 2013 waligundua walikuwa wanapunjwa mishahara kulingana na viwango vya serikali vilivyowekwa kwa malipo ya siku.

"Tunashukuru serikali kwa jitihada zao zote za kukubali kuwasimamia wananchi wake na kwa kumbana mkandarasi awalipe madai wafanyakazi wake," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, James Ihunjo, alisema hadi sasa wafanyakazi 109 waliolipwa ni wale ambao saa zao za kazi zilikuwa chini ya siku 500 na wale waliozidi siku hizo na makundi mengine yaliyojitokeza wataendelea kusikilizwa.


Nipashe
# TESA
Jumanne Juni 23, 2020
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14
**Mwanzo wa kutuliza mivutano karo, vifaa kinga**



Ukurasa 13
Wadau: Udhalilishaji wa watoto Zanzibar sasa unakaribia 'baibai'



Ukurasa 12
**Umewahi kujiuliza itakuwaje kama misitu itamalizika?**

ELIMU

## NA SABATO KASIKA

# Mvutano CWT, Chakamwata

• Mtihani kwa walimu pakukimbilia

WALIMU wana malalamiko kadhaa ambayo yanawafanya wasiridhike na asasi zinazosimamia maslahi yao, wakiamini kwamba hayapatiwi ufumbuzi na kusababisha wengine kufikiria kujitoa uanachama wa taasisi hizo au kufuata utaratibu mwingine.

Ndiyo maana hivi karibuni changamoto za kutorodhika na makato ya michango yao zimesababisha baadhi ya walimu kuibuka na chama kingine kwa ajili ya kutetea maslahi yao.

Malalamiko ya makato ya asilimia mbili ya mshahara kwa kila mwanachama na mchango wa rambirambi wa Sh. 200,000 zinazotolewa na Chama cha Walimu (CWT) mwanachama akifariki na kuzawadiwa mabati 20 akistaafu wanaamini kwamba, kiasi hicho hakitoshi ikilinganishwa na michango ambayo wamekuwa wakitoa katika chama hicho, pia mabati 20 ambayo mwanachama hupewa kama zawadi anapostaafu nayo hayatoshi.

Mbali na hayo, walimu wamekuwa wakidai kwamba, wakati mwingine hata hayo mabati 20 hayatolewi kabisa na kusababisha kuwapo kwa malalamiko yasiyoisha ndani ya CWT.

Ndiyo maana wapo baadhi ya walimu waliamua kuanzisha chama kingine kiitwacho Chama cha Kutetea Haki na Maslahi ya walimu Tanzania (Chakamwata), ambacho kinapingana na CWT.




Baadhi ya walimu wakiwa kwenye moja ya maadhimisho ya siku yao.

**KUWAPO KIZUNGUMKUTI**

Katibu Mkuu wa Chakamwata, Meshack Kapange, anadai kwamba walimu wengi siyo wanachama wa CWT na hawajawahi kuwa wanachama wa kisheria hivyo kuwakata mishahara yao kunazua jambo.

"CWT ilitumia nafasi ya kuwa chama pekee cha walimu kwa kuagiza makato ya asilimia mbili kwenye mishahara ya walimu wote nchini, siyo kama ada ya uanachama," anasema Kapange.

Anaongeza kuwa wengi na hususan walimu, wamekuwa wakihoji na kutafuta ukweli kuhusu mazingira na matukio yaliyosababisha kuanzishwa kwa CWT na madai mengine muhimu kwa maslahi ya wanachama.

"Hiyo ndiyo iliyosababishwa kuanzishwa kwa Chakamwata kwa ajili ya walimu wote wanaopenda kuona malalamiko yao yanapatiwa ufumbuzi wa kudumu ingawa safari yetu ina vikwazo vingi," anasema.

Anasema, chama hicho kinajulikana na kinaendelea kufanya taratibu za kujitambulisha mikoani na kusajili wanachama.

Wanachama hao wanasajiliwa kwa mujibu wa taratibu za sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini namba 6 ya mwaka 2004 na kanuni zake za mwaka 2007.

Katibu mkuu huyo anasema, Chakamwata kilipata usajili rasmi



Katibu Mkuu wa Chakamwata, Meshack Kapange

Machi 18 mwaka 2015, kwa lengo la kuwa mbadala wa CWT katika kutetea maslahi ya walimu nchini.

Baadhi ya wanachama (majina tunayo), wanazungumzia ubadhirifu na matumizi ya kufuru ya pesa za chama wakitaja kufanya burudani nje ya nchi na madai ya kuwapo kiburi na dharau kwa walimu.

Aidha, bungeni wabunge walihoji taarifa za jengo la Mwalimu House mali ya CWT na kueleza kuwa kuna benki imepangishwa na wapangaji wengine lakini haijulikani pesa za mapato zinaratibiwa na nani.

Kadhalika walimu hao wanalazimishwa kuingizwa kwenye chama cha kuweka na kukopa (Saccos ya Walimu) bila utaratibu wa kisheria na unaoelweka.

**MTAZAMO CHAKAMWATA**

Anasema, pamoja na CWT kufanya uchaguzi wapya, bado malalamiko ya walimu yatakuwa pale pale na kwamba yanaweza kuisha iwapo chama mbadala na serikali vitashirikiana kuyatatua.

"Chama chetu kimeanzishwa kwa ajili ya kutetea maslahi ya walimu, hivyo bila chama hiki, ninaamini kwamba malalamiko kuhusu maslahi ya walimu yataendelea kuwapo," anasema.

Kapange anadai kwamba, hiyo ni kwa sababu haoni kama CWT inaweza kuwavusha walimu na kuwafikisha katika hali bora na kufanya kazi yao bila manung'uniko.

"Serikali inapofikia kuitaka CWT kuchagua viongozi bora na waadilifu, maana yake ni kwamba imeiona kuna jambo haliko sawa na ndiyo maana sisi tukaainisha chama hiki baada ya kuona kero za walimu hazitatuliwi," anasema.

Anasema, malalamiko ya walimu hayawezi kutatuliwa na CWT kwa madai kwamba chama hicho ni sehemu ya matatizo ya kuendelea kuwapo kwa malalamiko hayo yasiyo na mwisho.

Kauli hiyo inaonyesha kuwa viongozi wapya wa CWT wana kazi kubwa ya kuunganisha walimu na kusimamia maslahi yao, ingawa Chakamwata haiamini kwamba hilo litawezekana

**CWT WANASEMAJE?**

Kwa upande wa CWT imepata viongozi watakaoiongoza kwa miaka mitano ijayo, wakiwamo wale walioteteа nafasi zao baada ya uchaguzi uliofanyika hivi karibuni.

Katika mazungumzo yake na gazeti hili, Katibu Mkuu wa CWT, Deus Seif, anasema, chama kitaendelea kusimamia katiba, kanuni, taratibu na sheria zake kwa maslahi ya wanachama kama ambavyo imekuwa ikifanya.

|Hata hivyo, akijibu malalamiko ya kutoa Sh. 200,000 za rambirambi ya mwanachama akifariki dunia, kuchelewesha au kutotoa bati 20 za kiinua mgongo na malalamiko ya kukata asilimia mbili ya mshahara, hakuwa tayari kuzungumzia kero hizo.

Licha ya kwamba kuna malalamiko mengi na maswali kwa CWT, Seif anaahidi kuwa wataongoza chama kulingana na katiba yao.

Anaongeza:"Kwanza kabisa sihitaji kuzungumzia Chakamwata, bali sisi ni viongozi tuliochaguliwa tutaendelea kusimamia wajibu wetu bila kutoka nje ya katiba, kanuni,taratibu na sheria."

Anasema, walimu wote ni wamoja na wanatakiwa kuungana na kufanya kazi inavyotakiwa huku wakitambua kuwa lengo ni kuinua kiwango cha elimu nchini, lakini pia wakipata maslahi yao inavyotakiwa.

Anasema, hakuna haja walimu kutengana wakati wanajenga nyumba moja ambayo ni maendeleo ya elimu nchini, hivyo ni vyema wadau wote ambao kimsingi ni walimu, wakalitambua hilo.

"Sisi walimu tuna jukumu kubwa la kuhakikisha Tanzania inakuwa na wasomi kuanzia ngazi ya chini hadi taifa, hivyo suala la kuwa wamoja ni la muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu," anasema Seif.

SAYANSI

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Umewahi kujiuliza itakuwaje kama misitu itamalizika?

WATANZANIA, bila kujali wewe ni mwanamke au mwanaume, au unaingia jikoni kupika au unanunua chakula gengeni umewahi kujiuliza swali hili;

"Hivi itakuwaje iwapo misitu ikimalizika baada ya kukataka kuni na kuchoma mkaa, familia na tasisi zitapikia nini?"

Kama hujawahi ni wakati wa kujiuliza kwa sababu kila kukicha matumizi ya kuni na mkaa kupika chakula yanaongezeka jambo linalooashiria kuwa misitu inateketea kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira unatokana na ama kukata misitu kwa ajili ya ardhi ya kilimo au kuchoma mkaa na kupata kuni. Tatizo hilo, halijapatiwa ufumbuzi endelevu.

Licha ya kwamba linaweza kutatuliwa kwa mbinu nyingi lakini kinachoendelea leo hakileti matumaini kwa vile si ufumbuzi wa kudumu wala si endelevu hivyo serikali na wadau wana jukumu la kutafuta suluhu ya kudumu kwenye kupunguza uharibifu wa mazingira unaoletwa na mahitaji ya nishati za kupikia na ardhi ya kilimo.

Kukata miti kunaongeza makali ya athari ya mabadiliko ya tabianchi na kunaacha maswali yasiyo na majibu mfano hivi misitu ikimalizika watu watapikia nini nyumbani, shuleni, hotelini, vyuoni na kwingineko?

Kwa mujibu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Tanzania inatumia tani milioni 2.5 za mkaa kwa mwaka na asilimia 60% ya mkaa huo sawa na tani milioni 1.5 hutumika Dar es Salaam.

Aidha, mwongozo wa Mifumo Endelevu ya Nishati ya Miti (mkaa na kuni) Tanzania Mwongozo wa Mafunzo ya Awali wa mwaka 2018 unaeleza kuwa Afrika inatajwa kuzalisha asilimia 62 ya mkaa wote duniani ambao unakisiwa kufikia tani milioni 52.

Tanzania inashika nafasi ya saba kwa uzalishaji wa mkaa duniani, ikichangia asilimia tatu ya uzalishaji wa mkaa wote duniani, kwa kiasi cha zaidi ya tani milioni 1.6.

Aidha, mwongozo unasema kuwa mkaa huchangia zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 2.7 (takribani Shilingi bilioni 6.2 ) kwa mwaka kwenye uchumi wa Tanzania na ni chanzo kikubwa cha ajira na kipato mijini na vijijini.

Hata hivyo, mwongozo haungi mkono kiasi hicho cha mkaa kinachokatwa na kuteketea na kushauri kuanza mbinu za kukabiliana na hali hiyo na kuhimiza kuanzisha na kuwekeza kwenye shughuli za kisasa za kilimo misitu ili kuzalisha miti kwa wingi kwa muda mfupi.

Ni kuwekeza kwenye uzalishaji wa miti kwa muda mfupi ili kupata misitu na mapori kwa muda mfupi na kupunguza kasi ya jangwa.

Aidha, kutafuta vyanzo mbadala vya maisha na mapato ili kupunguza utegemezi kwenye matumizi ya miti. Hoja ni kuwekeza kwenye shughuli mbadala kama vile mazao ya chakula na ya biashara ili kujipatia fedha kwa ajili ya vyanzo ili kununua nishati mbadala kama gesi, mafuta ya taa na nishati jua nayo ni ya msingi.



Matumizi ya mkaa na kuni imekuwa chanzo kikubwa cha nishati inayotumiwa katika maeneo mbalimbali. Ndio chanzo kikuu kinachofilisi misitu nchini. **PICHA: MTANDAO.**

> "Hata hivyo, hali hiyo hutegemeana na idadi ya wateja wanaohudumiwa. Ni wazi kutumia randa ni faida kimazingira kuliko kutumia mkaa na kuni japo mbao zilizorandwa kupata vumbi hilo ni kiama cha misitu.

Yote hayo hayawezi kufanikiwa bila kutokomeza umaskini kupitia kutengeneza ajira nyingi na mbalimbali ili kuepusha kutegemea mkaa na kuni kwa muda wote kama nishati ya kupikia mijini na vijijini.

Ni wazi kuwa, shule nyingi na vyuo nchini, zinatumia kuni na mkaa kupika chakula cha wanafunzi. Si hivyo tu migahawa, hoteli, vibanda vya chps na huduma za baba na mamalishe zote hutegemea mkaa na kuni.

Katika maeneo mengi viwanda vya kuoka mikate vinatumia kuni, wachoma matofali vijijini nao kadhalika hutegemea kuni. Kwa hiyo suala la kuacha kuni na mkaa halijapata ufumbuzi mahususi.

Zipo mbinu zinazobuniwa na baadhi ya watu binafsi na wafanyabiashara wanaotumia mkaa ama kuni kupika vyakula ama vya jumuiya au vya biashara.

Mbinu mojawapo ni kutumia vumbi randa ambayo wakaanga chips jijini Dar es Salaam na sehemu nyingine wanaitumia, lakini nayo chanzo chake ni miti hivyo huiweka misitni hatarini.

Wajasiriamali wanaotumia vumbi hili wanasema ukishindilia vumbi randa kikamilifu kwenye jiko lenye ujazo wa lita 20 kunawezesha kukaanga chips kwa siku nzima ikilinganishwa na kiroba cha mkaa ambacho kingeweza kutumiwa kwa siku hiyo.

Hata hivyo, hali hiyo hutegemeana na idadi ya wateja wanaohudumiwa. Ni wazi kutumia randa ni faida kimazingira kuliko kutumia mkaa na kuni japo mbao zilizorandwa kupata vumbi hilo ni kiama cha misitu.

Pamoja na kutumia vumbi randa pia wapishi hawa wanapendelea pia kubana matumizi ya kuni kwa kutumia majiko banifu.

Majiko banifu ama sanifu hutumia mkaa kidogo ama kiasi kidogo cha kuni kwa muda mrefu na kufanikisha kupika vyakula vingi . Hata hivyo, jitihada hizi bado zinahusika na misitu na zinachangia kuharibu mazingira.

Habari njema ambayo imeanza tangu mwaka 2017 ni kutoka Shirika la Madini la Taifa (Stamico) linaloeleza kuwa limeanza kuuza makaa ya mawe kutoka katika mgodi Kabulo ili kukidhi mahitaji ya nishati kwa wateja wakiwamo wa viwanda vya saruji na nguo .

Makaa ya mawe yanatajwa kuwa baada ya kuboreshwa yanaweza kutumiwa kupikia vyakula nyumbani na popote kwenye migahawa, hotelini, magerezani na vyuoni.

Wataalamu wa Stamico, wanaweza kuyaboresha kwa kuyapunguza joto kwa vile yanatajwa kuwa yana joto kali la zaidi ya nyuzi joto 5,000 ambazo zinaweza kuunguza vyombo vya kupikia na kuharibu afya ya binadamu na pia mazingira ya watumiaji iwe ni kibiashara au nyumbani.

Kwa ujumla taifa linahitaji mikakati endelevu ya kulinda misitu na makaa ya mawe ndiyo mbadala.

Aidha, makaa hayo yana faida kwani yanaelezwa kuwa mtumiaji hahitaji kiasi kikubwa kama ilivyo kwa mkaa wa miti. Kipande kimoja cha ukubwa fulani kinaweza kupikia vitu vingi kwakuwa tangu kuwaka kwake mpaka kumalizika huchukua zaidi ya saa nane.

Kwa hiyo makaa hayo ni dawa ya kulinda na kuhifadhi misitu kwakuwa matumizi ya makaa ya mawe yanaondoa utegemezi wa misitu kama nishati pekee ya kupikia, nchini.

Serikali kupitia ushirika wa sekta ya umma na ya binafsi (PPP) zinawajibika kutafuta mkakati endelevu wa kutafuta nishati mbadala badala ya kuni na mkaa kwani kwa Dar es Salaam pekee huenda tani zaidi ya milioni 1.5 za mkaa huteketea kila mwaka na kwa wastani tani 125,000 za mkaa hutumiwa kwenye jiji hilo.

Kwa Tanzania nzima huenda zaidi ya tani milioni 10 za miti huteketezwa kila mwaka kwa ajili ya kupika.

Asasi za utafiti na uendelezaji nishati kwa mfano Tatedo ya jijini Dar es Salaam zimeweza kutafiti na kuzijua aina za udongo unaofaa kutengeneza jiko banifu zikiwezeshwa kupitia PPA pamoja na kushirikisha wataalamu Satamico huenda kukapatikana upenyo.

Kutumia makaa ya mawe kama mbadala wa mkaa na kuni na kutaongeza makaa hayo sokoni na kuboresha eneo lote la upishi mijini na vijijini.

Hali hiyo itaendelea kuhifadhi misitu kwa faidi nyingi lakini pia kumaliza tatizo la ukosefu wa nishati ya uhakika.

Uwepo wa viroba vya mkaa pamoja na vibanda vya kuuza kuni kila mahali mijini hasa Dar es Salaam na miji mikubwa kama Dodoma ni kitisho kinachoonyesha kuwa kama jitihada hazitafanywa pengine miaka 10 ijayo nchi haitakuwa na miti lakini pia kutakuwa na tatizo la kutisha la kukosekana nishati ya kupikia.

Licha ya jitihada nyingi za kuhusisha PPP kuelekezwa kwenye kilimo ni wazi kuwa kuna haja ya kuwa na nguvu ya ziada kwenye nishati jadidifu kwani ni lazima kula na kutumia moto nyumbani na kwenye taasisi nyingine za umma na binafsi.

Viongozi wa serikali pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) msifurahie kununua mkaa njiani mnapopita na mashangingi na V8 na DFP badala yake kufanyike kazi zaidi kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa uharibifu wa mazingira.

Serikali na wadau wa PPP wawekeze vya kutosha kwenye miradi ya utafiti wa nishati mbadala na utafiti wa kupata misitu chapchap tena uwe endelevu huku kila mmoja akijiuliza hivi misitu ikimalizika watu wa taifa hili watapikia nini? Wataishije?

ELIMU

NA BEATRICE PHILEMON

# Wadau: Udhalilishaji wa watoto Zanzibar sasa unakaribia 'baibai'

UDHALILISHAJI na unyanyasaji watoto wa kike na kiume Zanzibar unaelezwa kuwa unaanza kupungua hivi sasa kutokana na mwamko mkubwa wa jamii kuripoti matukio ya vitendo vya udhalilishaji katika dawati la jinsia, polisi.

Aidha taarifa hizo pia hufikishwa katika vituo vya mkono kwa mkono 'one stop centres,' ambavyo vipo katika kila hospitali ya rufani ya mkoa.

Kwa mfano Zanzibar hupatikana hospitali ya mkoani, Pemba viko Chakechake, Micheweni na wilaya ya Wete Pemba kote huku kuna vituo vya mkono kwa mkono vya kusaidia watu kuripoti matukio hayo.

Kumekuwa na mwamko mkubwa wa kuripoti baada ya jamii kufundishwa elimu ya ulinzi na hifadhi ya mtoto na kufahamishwa kikamilifu kuhusu udhalilishaji, ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto na elimu ya malezi kwa watoto.

Pia walezi kupatiwa elimu ya kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Akizungumza na Nipashe Mratibu Mpango wa Kuimarisha Familia Pemba, wa kijiji cha SOS Children's Village Zanzibar, Gharib Abdallah, anasema kwa sasa kuna mambo ya kufurahisha kwenye kupambana na unyanyasaji.

Anaeleza kuwa mpaka sasa kituo cha SOS Zanzibar kinahudumia watoto111, wapo vijana 78 na mama walezi 13. Anasema hivi sasa unyanyasaji au udhalilishaji uliopo Zanzibar ni watoto kupigwa sana na masuala ya kukosa matunzo.

"Kama wadau wa kutetea haki za watoto mara nyingi tunatoa elimu kupitia mabaraza ya watoto ili wajue haki zao, kujua dhana ya unyanyasaji na jinsi ya kuripoti katika vituo husika vya masuala ya kukabiliana na ukatili," anasema.

Mbali na hilo, pia kwenye ngazi ya familia anaeleza kuwa wanafanya mafunzo. Aidha, kadhalika ndani ya jamii nako wanawafunza walezi, wazazi na uma ili kutambua suala la udhalilishaji watoto, ukatili wa kijinsia dhidi yao na pia wanawapa mbinu za namna ya kuripoti matukio hayo.

"Tumeamua kujikita katika eneo hili kwa sababu watu wengi Zanzibar hawajui sehemu sahihi ya kupata huduma. Kwa mfano, wazazi ndiyo wanasaidia watoto kupata haki zao na namna ya kuzipata," anasema Abdallah.



Ofisa Wanawake na Watoto Wilaya ya Chake Chake Pemba, Salma Khamis -Haji, akifundisha walezi na wazazi masuala ya kupambana na udhalilishaji wanawake na watoto: **PICHA: SOS ZANZIBAR.**

### ELIMU YA MALEZI

Mbali na hilo pia Abdallah anasema wanatoa elimu ya malezi bora kwa watoto na mpaka sasa wamefikia kata 15 na wameanza kutoa elimu hiyo kazi iliyoanza mwishoni mwa mwaka 2019.

Akielezea kile wanachofanya kusaidia watoto hao, anasema ni kutekeleza mikakati ya kumkinga mtoto na madhara ili asipate udhalilishaji na kuwasaidia wasibaki mitaani.

"Aidha, tunawaingiza kwenye mradi wa watoto wanaopata elimu ili kujiendeleza na kufikia ndoto na malengo yao lakini pia kuwawezesha kupata matibabu kwa huduma za mfuko wa bima afya. Mpaka sasa kuna watoto ambao tumewasaidia kupata kadi za bima ya afya," Abdallah anasema.

Watoto 300 wamepatiwa kadi za mfuko wa bima ya afya zenye thamani ya Sh. milioni 10.

Kwa upande wa elimu, watoto 1,800 wanasomeshwa kuanzia ngazi ya shule ya msingi, sekondari, vyuo vya ufundi na chuo kikuu na huduma hiyo imenza Januari mwaka 2019.

Mbali na kutoa elimu pia wanawapatia mafunzo ya ulinzi wa watoto ili watambue namna udhalilishaji ulivyo, athari zake, jinsi ya kuripoti matukio hayo na pia kuhusisha wadau kwani kama kamati inayohusika na masuala ya ulinzi na hifadhi ya mtoto.

Anasema elimu hii imeleta matokeo kwa Zanzibar kwa sababu vitendo vya udhalilishaji havitokei kwa kasi na hata kama vitatokea ni mara chache na jamii inachukua hatua kwa sababu watu hivi sasa wana hiyo elimu na wanachukua hatua za kuripoti hizo kesi.

### UKATILI KWINGINEKO

Abdallah anasema licha ya udhalilishaji kuripotiwa kuwa umepungua Zanzibar kuna baadhi ya sababu zinazochangia kuongezeka matukio ya uvunjifu wa haki za watoto nchini.

Anasema kuwa kuna baadhi ya matukio yanafanywa na wanafamilia na watu wa karibu na watoto na huku Zanzibar kuna kufichiana siri au kuoneana aibu au muhali.

Tatizo hili linarudisha nyuma juhudi za kuripoti matukio kwa sababu jamii inalindana na kuoneana aibu mambo yanayofanyika sehemu nyingi.

Kitu kingine kinachochangia uvunjifu wa haki za watoto ni baba na mama kutengana, anasema Abdallah na kuongezeka kuwa yote husababisha kunyanyaswa.

Akielezea mipango yao ya baadaye anasema ni kuwafikia watoto wengi zaidi hasa kwenye wilaya ambazo hawajawahi kufika ili wapate huduma ya malezi bora na haki zao za msingi.

Anasema watakuja na miradi mingine tofauti ili kufikia watoto wengi zaidi ambao wanaishi katika mazingira yanayosababisha kukosa haki zao kwamba lengo lao ni kumsaidia mtoto mwenye changamoto ya malezi bora.

### MIRADI MINGINE

Akielezea miradi inayotekelezwa na SOS anasema hivi kuna miradi tofauti ambayo inalenga kusaidia watoto katika jamii kupata haki zao katika jamii ikiwemo mradi wa kuimarisha familia Pemba na malezi mbadala na mradi mwingine ambao unatekelezwa katika wilaya ya Tumbatu mkoa wa Unguja.

### MCHANGO WA SERA

Zanzibar ina sera na sheria zinazosimamia ulinzi na ustawi wa mtoto ambazo zinahusika na masuala ya kumpa mtoto na haki zake za msingi.

Sheria hiyo ni namba 6 ya mwaka 2011, ambayo inashughulika ustawi na haki za watoto ndiyo inayosimamia masuala yanayohusiana na kundi hilo.

Sheria inasema kila mtoto ana haki ya kuishi, kuendelezwa, kupata elimu na kulindwa dhidi ya vitendo vya udhalilishaji wa aina yoyote kimwili, kiakili, kingono na kisaikolojia.

Na pia inasema mtu yeyote atakaye fanya vitendo hivi atakuwa ametenda kosa kisheria kulingana na sheria ya mtoto.

Lakini vile vile Zanzibar kuna Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kumaliza Vitendo vya Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto (2017-2022).

Mpango unatekelezwa katika maeneo mbalimbali kuanzia kata hadi wilaya ambako kazi hufanyika kwa kushirikiana na kamati ambazo zimeundwa ili kusaidia utekelezaji wa mpango huu kuanzia kata, wilaya hadi mkoa.

### WANAKAMATI

Baadhi ya wajumbe wa kamati hizo wanaiambia Nipashe kuwa wanafanya vikao kila baada ya miezi mitatu ambavyo vinajadili utekelezaji wa mpango kazi na kuweka mikakati ya kutokomeza vitendo vya udhalilishaji.

Wanakamati hao wa asasi ya SOS wanaitaka jamii kuwa mstari wa mbele kuripoti vitendo vya udhalilishaji watoto vinapotokea.

Aidha, wanaishauri serikali kuendesha kampeni za kutoa elimu ya masuala ya vitendo vya udhalilishaji kwa sababu jamii haina uelewa kuhusu masuala haya na kuna baadhi ya kata Zanzibar taarifa hizo hazifahamiki na wengi hawafahamu kwa kiasi kikubwa.

Kadhalika wanaomba serikali kuharakisha upelelezi wa kesi zinazohusu masuala ya udhalilishaji wa watoto, hukumu na kufanikisha matumizi ya sharia katika kutetea haki zao.

Mbali na hilo pia wanaomba serikali iwasaidie kuboresha mifumo ya upatikanaji wa haki za watoto kuanzia dawati la jinsia, mahakama za watoto na vitengo vya ustawi wa jamii ambao wanapokea kesi za udhalilishaji wa watoto ili kuwapo na mahakama rafiki kwa watoto zinazotetea haki zao.

NA MICHAEL ENEZA

## SHULE ZINAPOANZA

# Umewadia mwanzo kutuliza mivutano karo, vifaa kinga

Kufunguliwa shule kuanzia mwisho wa mwezi Juni, ni hatua nyingine ya kurudisha maisha yaendelee kama ilivyokuwa kabla ya kuzuka kwa ugonjwa wa homa kali ya mapafu maarufu kama corona au COVID-19.

Ni hatua iliyochukuliwa kwa kuridhika kuwa hali sasa imekuwa ya kawaida na ni kama vile hakuna uwezekano wa virusi vya corona kufika huko, hivyo kufungua shule ni kuondoa wasiwasi wa kuwapo hatari hiyo.

Ilikuwa tofauti kufungua vyuo na kidato cha sita kwa sababu maalum, kwani wahusika wa ngazi hiyo ya elimu wamepevuka kiumri, siyo watoto au vijana wadogo.

Ambacho hakijatatuliwa au kinaendelea kujadiliwa ni kiasi gani kuna mwendelezo wa sera ya tahadhari kuhusu maambukizi, na kiasi gani suala hilo limeondolewa katika ajenda.

Ndiyo hapo tofauti hii ya kwanza inakuwa na umuhimu, kuwa unaweza kufungua vyuo na kidato cha sita chini ya uangalizi, ila ni tofauti wakati uamuzi unachukuliwa kuhusu shule kwa jumla, kuwa hapo tumejiridhisha kuwa hakuna uwezekano wa kuzuka kwa hali kama hiyo?

Suala la tahadhari linakuwa la ziada, halitazamwi kimsingi. Ndiyo maana kuna mvutano ambao hata katika ngazi ya kufungua shule kwa uangalizi ungekuwepo, yaani wajibu wa kuhakikisha mazingira stahili ya kinga dhidi ya kusambaa kwa virusi vya corona.

Ila kwa mantiki hiyo suala hili litachukua sura tofauti, kuwa mradi siyo vyuo na kidato cha sita waliofunguliwa kwa tahadhari ila shule zote, haitakuwa rahisi kusema kuwa suala la tahadhari bado lina kipaumbele. Kufungua vyuo na kidato cha sita kwa tahadhari ilikuwa ni mazingira ya kuhitaji au kutazamia vigezo vya tahadhari vichukuliwe kwa njia stahili, inayoweza kuwakinga wanafunzi kiuhalisi.

Kwa mantiki ya kuhitaji maisha yarudi katika hali ya kawaida, na shughuli ziendelee kama zilivyo na hivyo huduma hizo nazo zifunguliwe, ni wazi kuwa kinachodhaniwa kuwa ni tahadhari za msingi sasa ni kama kimepitwa na wakati.

Sababu ni kuwa huwezi kuwa na wanafunzi wote shuleni halafu tahadhari zinazofaa zikachukuliwa, kwani hata kwa upande wa vyuo na kidato cha sita ilikuwa wazi kuwa hofu halisi ya COVID-19 imepungua. Cha ziada ni kuwa wanaohusika hapo wamepevuka kiumri hivyo ni rahisi zaidi kufuata maelekezo kuhusu kujikinga na kuambukizwa kirahisi, hasa kwa kunawa, kuvaa 'barakoa.'



Ndivyo itakavyokuwa Jumatatu Juni 29, shule zikianza kwa wanafunzi shule za msingi kuvaa barakoa. **PICHA: MTANDAO**

> Suala la tahadhari linakuwa la ziada, halitazamwi kimsingi. Ndiyo maana kuna mvutano ambao hata katika ngazi ya kufungua shule kwa uangalizi ungekuwepo, yaani wajibu wa kuhakikisha mazingira stahili ya kinga dhidi ya kusambaa kwa virusi vya corona.

Ina maana kuwa kufunguliwa kwa shule kunaashiria kuwa hali imerudi kuwa ya kawaida na hivyo masuala haya ya kujikinga yanachukua sura ya sera ya afya na kwa upande mwingine ni staha ya kisiasa kuwa bado tunajali uwepo wa maambukizi ya corona.

Hili linaweza kuleta matatizo ya kiutaratibu endapo wizara husika zitaweka mkazo kuona kuwa maelekezo hayo yanafuatwa. Kinyume chake ni kukumbushana tu mara kwa mara katika majukwaa.

Tatizo ni kuwa katika hali ya kawaida isiyo na tahadhari zozote ambazo kuzitilia maanani kunazidisha gharama, wamiliki wengi wa shule na hasa vyuo na vyuo vikuu wanapata taabu kufikia viwango vya miundombinu vinavyohitajiwa.

Ndiyo sababu ya kufungwa kwa vyuo vikuu na taasisi nyingine kadhaa za elimu ya ufundi au ustadi kutokana na mapungufu ya wazi kati ya viwango halisi katika vyuo hivyo na viwango vinavyojitahiwa.

Tatizo hilo haliwezi kuwa limemalizika, hasa ukitilia maanani kuwa kuzuka kwa gonjwa la corona kumevuruga shughuli nyingi za uchumi na wengi waliopungukiwa na fedha kwa hali hiyo wanasomesha vijana wao vyuoni na shuleni hivyo hata uwezo wa ada ni hafifu.

Uwezo wa ada unapopungua ni kwamba hata taasisi hizo zitafanya kazi chini ya kiwango stahili kwa vipato vyao, yaani wanao walimu na madarasa lakini wanafunzi wamepungua, kwani baadhi wanashindwa kulipa ada.

Serikali inasisitiza kuwa karo za muhula wa kwanza wa masomo kwa mwaka huu ziwe zimekamilishwa ila wanafunzi wasizuiwe kuingia darasani au kupokelewa shuleni kwa kutokumaliza malipo ya muhula wa pili, yaani kukamilisha karo yote.

Kuna uwezekano pia wa misuguano kuhusu vifaa kinga kwa maambukizi ya corona, ingawa labda hilo litategemea kusikika kwa maambukizi mapya ambayo labda hayajasikika kwa muda.

Hata ikisikika kuna maambukizi mapya haitakuwa rahisi kurudi katika kufunga taasisi za elimu kwa jumla kwani kuna fikra tangulizi kuwa Watanzania wajifunze kuishi na ugonjwa huu kama yalivyo mengine, ila uwezekano wa kuzuia shule za msingi na sekondari hadi kidato cha nne unaweza kuwepo endapo hofu ya corona itaongezeka. Kufunga vyuo kama mwanzo itachukua hali halisi ya hatari.

Kimsingi ni kuwa kufungua vyuo na kidato cha sita kuliendana na uhakika wa wastani kuwa tishio la corona linaondoka kati yetu na siyo tishio tena kwa maana ya kujua kuwa watu wengi wataambukizwa katika siku za usoni nchini, kwa mfuatano wa takwimu au kusikia taarifa za vifo kawaida.

Kufunguliwa shule kwa jumla ilikuwa ni kielelezo cha kupotea kwa hofu hiyo kutokutazamiwa kuwa maambukizi yanaweza kupanda katika siku za usoni na hivyo maisha lazima yaendelee.

Ni hali ambayo hata kama tutaendelea kusisitiza umuhimu wa kujikinga, haiwezi kuhakikishwa kwa ngazi zote za elimu kwani hawana raslimali za kutosha kwa mahitaji hayo, na ulazima huo unapungua kila uchao.



Maisha yakirejea taratibu katika hali ya kawaida ndivyo mitaa ikiwamo Congo jijini Dar es Salaam itakavyoendelea na shughuli zake. **PICHA: MTANDAO.**





# Maabara kubaini ubora wa maji kabla ya kusambazwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeanzisha maabara itakayosaidia kujua ubora wa maji kabla ya kusambazwa kwa wananchi.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki jijini hapa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Prof. Kitila Mkumbo, alipokuwa akizindua maabara ya maji ya kisasa na kutoa vifaa vilivyotolewa kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Nguvu ya Atomiki (IAEA).

Aliagiza wataalamu wa maabara hiyo kuitumia kwa uangalifu kwa ajili ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji hapa nchini.

"Tunategemea maabara hii itatumika kuboresha huduma za maji kwa wananchi ili kuleta manufaa kwa Watanzania," alisema.

Alisema maabara hiyo ni ya muhimu sana katika wizara hiyo kwa kuwa itasaidia kufanya tafiti za upimaji maji ambazo zitafanywa ndani ya maabara.

"Naomba tutunze vifaa vya maabara hii ni vizuri na ni vya gharama hivyo ni vema kuvitunza ili na wengine waje wavitumie," alisema Prof. Mkumbo.

Prof. Mkumbo alisema kwa kutumia kifaa cha Isotope Hyrology kilichopo kwenye maabara hiyo, kina uwezo wa kujua jinsi maji ya juu ya ardhi yanavyovia ardhini na kuhifadhiwa katika miamba.

Naye Naibu Katibu Mkuu Wizara hiyo, Mhandisi Anthony Sanga, alitoa wito kwa taasisi za elimu na kampuni za sekta binafsi kupata ujuzi kupitia maabara hiyo ili kuiimarisha utendaji kazi wao.

Mhaidrojia Emanuel Nahozya, alisema maabara hiyo inaweza kujua ubora wa maji kwa kutambua maji hayo yana nini na kutibiwa kabla ya kusambazwa kwa wananchi kwa matumizi ya kibinadamu.

# Waziri ataka utatuzi wa matatizo ya wajane

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amesema asilimia 3.1 ya wanawake nchini ni wajane na kuhimiza wadau kuhakikisha wanashughulikia matatizo ya upatikanaji wa haki zao.

Rai hiyo ilitolewa na Kaimu Mkurugenzi Idara ya Jinsia wa Wizara hiyo, Grace Mwangwa, alipokuwa akisoma tamko la maadhimisho ya Siku ya Wajane Duniani kwa niaba ya Waziri Ummy.

Alisema kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu, inakadiria kuwa idadi ya wajane nchini ni 800,000 ambayo ni sawa na asilimia 3.1 ya wanawake wote nchini ambao wanakadiriwa kuwa milioni 28.5 kwa mwaka 2019.

Alisema pamoja na mambo mengine, maadhimisho hayo yanatoa fursa ya pamoja katika kubaini changamoto za wajane na namna ya kukabiliana nazo.

"Hivyo basi, Tanzania huadhimisha Siku ya Wajane kwa lengo la kujenga hamasa, mshikamano na uelewa ndani ya jamii ili kuacha ukiukaji wa haki za binadamu ambao hufanywa kwa wajane mara wanapokuwa wameachwa na wenza wao," alisema.

Alihimiza kila mdau kuchukua na kushughulikia changamoto za upatikanaji wa haki kwa wajane pamoja na kuwalinda ili wapate haki zao ikiwa ni pamoja na haki ya kumiliki ardhi, kurithi mali na ulinzi katika familia.

"Napenda kuwahimiza wadau wanaotoa huduma kuchangia katika uwezeshaji wa kiuchumi wa wanawake hasa kundi hili la wajane ili kuondokana na umaskini wa kipato katika kaya zao," alisema.

Kadhalika, alisema serikali imefanya jitihada mbalimbali za kuondoa kero zinazowakabili ikiwa ni pamoja na kuelimisha jamii kuacha mila na desturi kandamizi zinazofanywa kwa wajane ili wajikwamue kifikra, kiutamaduni, kiuchumi na kijamii.

"Kuweka na kuimarisha mifumo ya kulinda haki za wanawake wakiwamo wajane ikiwapo kuwekwa kwa mpango kazi wa Taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (MTAKUWA 2017/18 - 2021/2022) wenye lengo la kutokomeza ukatili kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2021/2022," alisema.

Pia alisema katika kutekeleza mpango kazi huo serikali imeunda jumla ya kamati 16,343 za ulinzi wa wanawake na watoto ili kuhakikisha kuwa vitendo vya ukatili vinatokomezwa.

"Taasisi 125 za kutoa huduma za msaada wa kisheria zimetambuliwa na wasaidizi wa kisheria 2,599 wamesajiliwa kote nchini na wanufaika wakubwa wa huduma hizo ni wanawake wakiwamo wajane," alisema.

Aidha, alisema kwa mwaka 2018/19 serikali ilitoa msaada wa kisheria kwa wajane na hivyo kesi 277 za mirathi ziliweza kutolewa hukumu ya ushindi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Chama cha Wajane (TAWIA), Rose Sarwat, aliwashauri jamii kuweka utaratibu wa kuandika wosia ili kuziondolea usumbufu familia pindi wanapofariki.



Mdau wa elimu, James Yuna, akizungumza na wanafunzi wa shule mbalimbali za sekondari, msingi na awali za jiji la Dodoma, wakati wa ibada maalum ya kumpongeza na kumshukuru Rais John Magufuli, kwa hatua yake ya kuzifungua shule, iliyofanyika katika Kanisa la Tanzania Assemblies of God, Maili Mbili, juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**.

# Waziri Ndalichako ataka kutunzwa kwa miundombinu chuoni

**Na Augusta Njoji,** MPWAPWA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako ameagiza kutunzwa miundombinu ya Chuo cha Ualimu Mpwapwa inayojengwa na kukarabatiwa kwa Sh. bilioni 2.8 ili itumike kwa muda mrefu.

Prof. Ndalichako alitoa kauli hiyo jijini hapa alipokuwa akizungumza na wakufunzi na wanafunzi baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa miundombinu ya chuo hicho.

Alisema uongozi na wanafunzi wa chuo hicho wanapaswa kusimamia na kuhakikisha miundombinu inatunzwa.

"Serikali imeamua kuwekeza katika uboreshaji wa miundombinu ya Taasisi za Elimu ili kuongeza fursa ya upatikanaji wa elimu kwa Watanzania," alisema.

Alitaja miundombinu inayojengwa ni jengo moja la ghorofa kwa ajili ya Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), bweni la ghorofa moja la walimu tarajali wa kike, bwalo la chakula na nyumba mbili za watumishi ambazo nyumba moja ina uwezo wa kuchukua familia tatu.

Alisema kwa sasa inaboresha miundombinu ya elimu ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

"Sasa ni jukumu lenu kusimamia na kuhakikisha miundombinu inatunzwa ili iweze kutumika kwa muda mrefu," alisema.

Naye Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya ya Mpwapwa, Said Mwaliego, alishukuru wizara kwa kutoa kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa chuo hicho na kuiomba kusimamia mradi huo kwa karibu ili ukamilike kwa wakati.

Kwa upande wake, Mkuu wa Chuo hicho, Gerald Richard, alisema miundombinu hiyo ilikuwa imechakaa kutokana na kuwa ya muda mrefu.

"Nashukuru wizara kwa kukipatia fedha za ukarabati chuo hichi kwani miundombinu yake ilikuwa imechakaa kutokana na kuwa cha muda mrefu na ukarabati huu tunategemea utaongeza nafasi za udahili wa wanachuo wengi zaidi."







Mchuuzi wa kuku wa kienyeji, akisaka wateja katika eneo la kituo cha daladala cha Kabwe, jijini Mbeya juzi, ili kujipatia ridhiki. Kuku mmoja aliuzwa kwa 7,000/- hadi 10,000/- kulingana na ukubwa wake. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**.

# Abiria, madereva mabasi wanaotupa taka kitanzini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (Latra) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, imesema inafuatilia madereva na makondakta wa mabasi ya mikoani kwa kutumia Mfumo wa Ufuatiliaji Mienendo ya Mabasi (VCT), ili kubaini wanaokiuka sheria za usafi wa mazingira kwa kutupa taka ovyo kwenye hifadhi za barabara na mapori.

Meneja wa Latra wa Kanda hiyo, Denis Daudi, aliyasema hayo juzi alipozungumza na Nipashe kuhusu utaratibu wa kudhibiti usafi kwenye mabasi, akieleza kuwa wamelazimika kutumia mfumo huo baada ya uchafuzi wa mazingira kuendelea kufanyika.

Alisema kuwa baadhi ya makondakta huwa wanatupa taka kwenye maeneo ambayo hayajatengwa kwa ajili ya shughuli hiyo licha ya kuelekezwa maeneo maalum ya kutupa taka.

Denis alisema utupaji ovyo wa taka hizo unasababisha magonjwa ya mlipuko na kuwadhuru wanyama, hivyo ni lazima utupaji huo wa taka udhibitiwe kwa nguvu.

"Tulitoa maelekezo na kutenga maeneo ya utupaji wa taka na kila basi lazima liwe na vifaa cha kutunza taka na abiria lazima waelekezwe kuweka taka humo lakini bado tatizo lipo, hivyo tunafanya uchunguzi wa kina kwa kutumia mifumo, ili kubaini wanaohusika na kuchukua hatua," alisema.

Aliwataka wamiliki wa mabasi kukaa na kuzungumza na makondakta na madereva ili wawaelekeze wafuate maelekezo wanayoyapata kutoka katika idara za serikali na kwamba katika Mkoa wa Mbeya tatizo la utupaji ovyo wa taka lilikuwa katika eneo la Igawa wilayani Mbarali.

Baadhi ya wananchi waliviomba vyombo mbalimbali vya serikali vinavyohusika na shughuli za usafirishaji, kusaidia kudhibiti utupaji ovyo wa taka kwenye maeneo mbalimbali.

Mmoja wa wananchi hao, Selina Joram ambaye ni mkazi wa Jiji la Mbeya, alisema suala la usafi linapaswa kupatiwa kipaumbele kwa kukagua mabasi yanapoanza safari na kila kituo kuwapo na ukaguzi, ili kuwabaini makondakta wakorofi na kuwachukulia hatua.

Maofisa usafirishaji wa mabasi walidai huwa wanahakikisha mabasi yao yana vitunza taka, lakini tatizo huwa ni baadhi ya abiria kuwa wakorofi kwa kutupa taka kupitia kwenye madirisha.

Mmoja wa maofisa hao, Saco Sinapesa, alisema huwa wanatoa elimu kwa abiria, lakini wengine huwa wanakiuka kwa makusudi na wengine wanajisahau na hivyo akaiomba Latra kuutumia mfumo huo kuwashughulikia pia abiria wanaobainika kutupa taka.

"Tunatoa elimu lakini unakuta abiria wengine wanakaidi kwa makusudi maelekezo na wanatupa taka madirishani, tunaomba serikali itusaidie kuwashughulikia maana wanaoumia ni sisi badala ya abiria wanaokiuka," alisema.

# Wabaini faida kula viazi lishe

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wa viazi lishe kwenye Bonde la Songwe katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameomba serikali kutoa elimu kwa wananchi kutumia viazi hivyo kama chakula kwa watoto kutokana na kuwa na faida nyingi kiafya.

Wakizungumza na Nipashe juzi, baadhi ya wakulima hao walisema viazi hivyo vina vitamini na madini ambayo ni muhimu kwa ukuaji wa watoto ikiwamo Vitamini A.

Mmoja wa wakulima hao, Joseph Mshani, alisema walianza kulima viazi hivyo baada ya kupatiwa elimu na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Kituo cha Uyole ambao waliwapa mbegu na kuwafundisha namna ya kulima.

Mshani alisema wamekuwa wakivitumia viazi hivyo kwa ajili ya chakula na biashara na kwamba kwa sasa vimeanza kuwa na soko zuri kutokana na baadhi ya wananchi kuanza kuelewa faida zake na hivyo akaiomba serikali kuongeza elimu kwa wananchi.

"Tunatengeneza juisi ya viazi hivi na kuiuza, lakini wakati mwingine tunaviuza hivi viazi, ili mtu akapike ama achome, pia huwa tunawafundisha faida za viazi hivi wateja wetu," alisema.

Roda Chaghi, mkulima mwingine katika bonde hilo, alisema kuwa tangu aanze kulima viazi hivyo miaka miwili iliyopita, amepata faida kubwa ikiwamo ya kiuchumi na afya kwa watoto wake.

Alisema viazi hivyo vimemsaidia kununua kiwanja na kujenga nyumba na kwamba ana uhakika elimu ikitolewa kwa wananchi juu ya faida za viazi hivyo, kuna uwezekano akapata faida kubwa zaidi.

# AGRICOM yatahadharisha wakulima zana duni kilimo

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

TAASISI ya AGRICOM Afrika LTD inayojihusisha na usambazaji wa zana mbalimbali za kilimo, imewataka wakulima nchini kuachana na matumizi ya zana duni za kilimo likiwamo jembe la mkono na badala yake watumie zana za kisasa ambazo zitawasaidia kulima maeneo makubwa na kuongeza tija.

Rai hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na mwakilishi wa taasisi hiyo, Cecilia Julius wakati wa Mkutano wa Asasi ya Uwezeshaji wa Sekta Binafsi ya Kilimo (Pass Trust) na wadau wa kilimo, mifugo na uvuvi.

Cecilia alisema kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia yanayoendelea duniani, Watanzania wanatakiwa kuendana nayo ili kuwa na uwezo wa kuzalisha mazao kwa wingi na kuongeza kipato.

Alisema taasisi hiyo ina mashine mbalimbali za kisasa ambazo zinafanya kazi kuanzia kwenye uandaaji wa mashamba mpaka kwenye uvunaji, hivyo zinarahisisha kazi na kumfanya mkulima kulima eneo kubwa kwa wakati mfupi.

"Hizi mashine tunaziuza kwa pesa taslimu ama kwa mkopo na tumeshajiunga na wenzetu Pass Trust, ili kuwarahisishia wananchi upatikanaji wa mikopo ya vifaa vyetu kwa sababu wenzetu hawa wanadhamini mikopo kwa wakulima," alisema.

Cecilia alizitaja baadhi ya mashine ambazo taasisi hiyo inazo kuwa ni matrekta, 'combine' za kuvunia, majembe ya kuvutwa na ng'ombe pamoja na mashine za kupandia mahindi na mpunga.

Aliwashauri wakulima kuchangamkia mikopo ya vifaa hivyo kwa maelezo kuwa urejeshaji wa mikopo hiyo ni wa taratibu na baadhi inachukua miaka kadhaa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Pass Trust, Nicomed Bohay, alisema wanashirikiana na taasisi hiyo na Benki ya Maendeleo ya Kilimo kuwasaidia wakulima kupata mikopo.

Alisema ili mkulima asaidiwe na Pass kukopeshwa mashine ama pesa, ni lazima awe na uwezo wa kujidhamini kwa angalau asilimia 20 ya mkopo wote na kwamba asilimia nyingine inayobaki anadhaminiwa na Pass Trust.

"Wenzetu AGRICOM wanasambaza hizi zana za kilimo, lakini taasisi za fedha zinakopesha pesa, hivyo tukiziunganisha taasisi zote hizi, tuna uhakika wa wakulima wetu kuongeza uzalishaji," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alizishauri taasisi zote zinazotoa mikopo kwa wakulima katika mkoa huo kuweka masharti nafuu, ili kuwawezesha wakulima wengi zaidi kukopa kwa ajili ya maendeleo ya kilimo na uchumi.

Aliishauri AGRICOM Afrika kuziuza mashine zake kwa bei nafuu, ili wakulima wengi zaidi wamudu kuzinunua na kuzitumia kwenye uzalishaji.





# Wananchi waondolewa hofu uchaguzi mkuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAKATI uchaguzi mkuu ukitarajiwa Oktoba mwaka huu, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Yussuf Masauni, amesema vyombo vya ulinzi na usalama vitahakikisha vinasimamia vyema shughuli zote za uchaguzi ili wananchi waweze kutumia haki yao ya demokrasia ya kupiga kura kwa hali ya amani na usalama.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kukutana na maofisa wa Jeshi la Polisi mjini hapa alisema kuwa katika kuelekea katika uchaguzi mkuu hali ya amani na usalama itazidi kuimarika na kuwataka wananchi waendelee kushiriki katika harakati za uchaguzi bila ya hofu.

"Niwatoe hofu wananchi katika kipindi hiki cha kuelekea katika uchaguzi mkuu, waendelee kushiriki katika harakati za uchaguzi, wanaoamua kugombea wagombee nchi hii itaendelea kuwa salama," alisema.

Alilipongeza jeshi hilo kwa kazi nzuri ya kulinda usalama wa wananchi wa Zanzibar na wageni ambayo imesaidia kupungua kwa vitendo vya uhalifu.

Naye Kaimu Kamishna, Awadhi Juma Haji, alisema jeshi hilo limeshajipanga kikamilifu katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu na kuhakikisha unafanyika katika hali ya amani na utulivu.

Alisema kuanzia kampeni, upigaji kura na kutangazwa kwa matokeo, jeshi hilo litahakikisha matukio hayo yanafanyika kwa hali ya amani na usalama.

"Tunataka wananchi watumie haki yao ya kikatiba na kidemokrasia na wale wagombea kufanya kampeni kwa amani na usalama," alisema.

Aliwataka wananchi kuendelea kutii sheria za nchi bila ya kushurutishwa na yeyote atakayekwenda kinyume na sheria za nchi jeshi hilo atachukuliwa hatua kali kwa mujibu wa sheria.

Alisema kuwa hawataruhusu vitendo vya uvunjifu wa amani kutokea au mtu yeyote kutumia kisingizio cha mambo ya siasa kufanya matukio ya uhalifu.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, akikalia moja ya viti vilivyotolewa na serikali kwa shule za Zanzibar, wakati wa hafla ya kukabidhi jana. **PICHA: OMPR – ZNZ.**

## Mwana-CCM asiyeshiriki uchaguzi kunyang'anywa kadi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Kaskazini, Unguja Ame Ali Iddi, amesema mwanachama wa chama hicho ambaye atapuuza na kushindwa kushiriki katika uchaguzi mkuu wa Oktoba bila ya sababu za msingi atanyang'anywa kadi ya chama.

Iddi alisema hayo wakati alipozungumza na kamati ya shule katika makabidhiano ya madawati kwa shule za Jimbo la Mkwajuni Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema Katiba ya CCM inasisitiza ushindi katika uchaguzi wote kuanzia shina, matawi hadi uchaguzi mkuu wa taifa kwa ajili ya kushika dola.

Alisema kitendo cha mwanachama kukataa kushiriki katika uchaguzi mkuu na kupiga kura, hakikubaliki katika mkoa huo kwa sababu wamejipanga kuchukua majimbo yote ya uchaguzi ya mkoa huo.

"Tumefanya uchaguzi na kubaini kwamba wapo wanachama wetu wakati wa kipindi cha uchaguzi mkuu hawashiriki kupiga kura huku wengine wakiwa hawana sababu yoyote... Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Kaskazini Unguja hakitakubali uamuzi huo watu wa aina hiyo tutawanyang'anya kadi kwa sababu hana nia njema na chama," alisema.

Naye Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni, Ussi Yahya, alisema kuwa katika kipindi cha miaka mitano ya uongozi amejitahidi kutekeleza ilani ya chama kuwaletea maendeleo wananchi wa jimbo hilo.

# Balozi Iddi atahadharisha uvamizi maeneo yaliyotengwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Iddi, amesema uvamizi wa ujenzi holela wa majengo ya kudumu katika maeneo ya serikali waliyopewa wananchi mwaka 1964 kuendeleza kilimo ukiachwa unaweza kuleta athari.

Alisema masheha pamoja na watendaji wa halmashauri za wilaya, lazima waelewe kwamba watabeba dhima dhidi ya kasi hiyo ya ujenzi inayofanyika ndani ya macho yao ambayo inakwenda kinyume na falsafa ya Muasisi wa kwanza wa Mapinduzi ya Zanzibar, marehemu Mzee Abeid Amani Karume.

Alisema hayo wakati akizungumza na wananchi, kamati za shule na walimu wa Jimbo la Mahonda, katika ziara yake maalum ya kukabidhi meza na viti shule nne za jimbo hilo ikiwa ni mgao wa serikali kufuatia kampeni maalum ya kuondoa tatizo la madawati kwa shule za Zanzibar.

Alisema tamaa ya baadhi ya viongozi wa halmashauri pamoja na shehia kwa kuhusika katika masuala ya uuzaji wa ardhi hasa maeneo ya eka yataumiza kizazi cha sasa na kijacho kwa kukosa maeneo ya kuendeleza miradi ya maendeleo katika sekta ya kilimo.

Balozi Iddi alisema wapo baadhi ya watu walioamua kuendeleza kampeni ya kutumia fedha nyingi kwa kununua eka za serikali zilizotolewa kwa kilimo wakiwa na mkakati maalum wa kujirejeshea maeneo hayo kwa mlango wa nyuma wakati Serikali Kuu tayari imeshayataifisha tangu mwaka 1964.

Alisema serikali haitasita kumchukulia hatua za kisheria mtu au kiongozi yeyote atakayebainika kujihusisha na masuala ya uuzaji wa eka za serikali hatua itakayokwenda sambamba na kunyang'anywa maeneo hayo mtu aliyeuziwa na kuyarejesha serikalini.

Akizungumzia suala la madawati, Balozi Iddi, alisema lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwapunguzia usumbufu wanafunzi wake kutokana na changamoto kubwa inayowakabili ya uhaba wa madawati.

Alisema kitendo cha wanafunzi kuendelea kusoma bila madawati kinarudisha nyuma maendeleo ya elimu hasa ikizingatiwa kwamba mwanafunzi wa karne ya 21 lazima aende na wakati wa sasa wa mfumo wa Sayansi na Teknolojia.

Naye Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Kaskazini Unguja, Iddi Ali Ame, alisema wakati umefika kwa walimu wa shule zilizomo ndani ya mkoa huo kurejeshea heshima yake kwa matokeo mazuri ya ufaulu wa wanafunzi.

Iddi alisema kipindi cha miaka mitatu iliyopita mkoa huo pamoja na wilaya zake zimeshuhudiwa kuwa na matokeo mabaya ya wanafunzi, jambo ambalo kwa sasa viongozi hawapendi kulishuhudia kutokana na nguvu kubwa ya serikali iliyofanywa ya kuwapunguzia changamoto zao ikiwamo upatikanaji wa madawati.

Kwa upande wao, walimu wakuu na wenyeviti wa kamati za shule hizo, wameipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutekeleza ahadi yake iliyotoa ya kuondoa changamoto za madawati iliyokuwa ikiwakabili wanafunzi hao wa shule za msingi.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**NAFASI ZA KAZI YA DEREVA NA MAUZO** Mwenye uzoefu wa kuuza Maji. PIga simu namba : **0767 269677 saa za kazi**


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA CHETI



**Titus Michael Kisandu** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S4934-0102** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2016 katika shule ya Sekondari Mwayunge. Yeyote atakae kiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi Taarifa: **IGU/RB/1145/19**

115784202

## KUPOTELEWA NA LESENI

**MAULIDI MASUDI MUHOMBA** anatangaza kupotelewa na Leseni ya uchimbaji wa madini **(Primary Mining Licence)** yenye namba ya usajili **001909WZ** iliyopotea tarehe **20.05.2019.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KAS/RB/4267/2019.**

115785102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;156/2020**

**Ombi la JUNES CHIBUNDU KIBONA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu EZEKIEL ULISUBISYA KIBONA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 02/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 17/06/2020.

Tarehe 17/6/2020

Sahihi ya Hakimu

HAKIMU

MAHAKAMA YA MWANZO MJINI MOROGORO

115785002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FOMU II (S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya NYALIKUNGU (W) MASWA**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 12/2020**

**Ombi la MARIA CHARLES JILASA kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu EMANUEL PAUL MAHEGA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 15/07/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo .
Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 15/06/2020.

MAHAKAMA YA MWANZO WILAYA YA MASWA

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO

115784102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;159/2020**

**Ombi la UKENDE PAUL UGULA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu STANLEY PETER MGULUMBI**


Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 06/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 22/06/2020.

Sahihi ya Hakimu

MAHAKAMA YA MWANZO MOROGORO

115785502

## KUPOTEA KWA CHETI



**FIDEA REGNARD KOMBA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NAMBA **S.3126/0007** KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA KUPITIA LULI SEKONDARI MWAKA 2017.YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA YA POLISI **RUV/MBI/RB/259613/2020**

115783602

## KUPOTELEWA NA KADI ZA GARI

**NASSRA MOHAMED SULTAN** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI ZA GARI ZENYE NAMBA ZA USAJILI **T433 DPT** AINA YA **FAW** YENYE CHASSIS NO **LFWNHXPHXJAD46899** NA ENGINE NO **1618J125879.** TAARIFA YA POLISI **KAH/RB/220/2020** NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 431 DPT** AINA YA **FAW** YENYE CHASSIS NO **LFWNHXPH2JAD46900** NA ENGINE NO **1618J126348.** KWA YOYOTE ATAKAYEZIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI **KAH/TR/RB/221/2020.**

115785202

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYANI KAHAMA**

**MAOMBI YA ARDHI NAMBA 30 YA 2016**

**PETER KAWANA....................................MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **SADA NASSORO**
2. **HASSAN MWENDO**
3. **MBUGA SITTA**
4. **FADHILI HASSAN ATHUMANI.....................WAJIBU**

**KWA; HASSAN MWENDO**
**FADHILI HASSAN ATHUMANI**

**TAARIFA YA KUITWA SHAURINI**

MNAJULISHWA KWAMBA MNAMO TAREHE 30 /7/ 2020 SAA 3;00 ASUBUHI SHAURI TAJWA HAPO JUU LIMEPANGWA KUSIKILIZWA NA MWENYEKITI WA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA MHE, CHRISPIAN HATSON .

HIVYO MNA AMRIWA KUHUDHULIA SIKU HIYO KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA KAHAMA BILA KUKOSA ,MBELE YA MAWAKILI AU WAKALA WANAOTAMBULIKA KUSIKILIZA SHAURI.
ZINGATIA TANGAZO NA FUATA MUDA NA TAREHE TAJWA HAPO JUU, IWAPO HUMTAFIKA, SHAURI LITASIKILIZWA BILA YA KUJALI KUTOKUWEPO.

HATI HII IMETOLEWA KWA AMRI YANGU NA KUPIGWA CHAPA NA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA KAHAMA TAREHE 10/6/ 2020.

CHAIRMAN

115785302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;160/2020**

**Ombi la HALIMA ABDALLAH PINTO Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ABDALLAH RAMADHAN PINTO.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 02/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe ......../20.....

115785602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;162/2020**

**Ombi la KONGERA MOHAMED CHASSAMBA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu MOHAMED MRISHO CHASSAMBA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 02/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 22/06/2020.

115785902

## KUPOTEA KWA CHETI



**MONICA FILOTEUS NDOMBA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE **INDEX NAMBA S.3126/0010** KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA KUPITIA LULI SEKONDARI MWAKA 2017. YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA YA POLISI: **RUV/MBI/RB/259250/2020.**

115783702

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**STEVEN SAITOTI TARAKWA** Anatangaza kupotelewa na **kadi ya pikipiki** yenye namba za usajili **T285 APE** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi Taarifa **ARU/ARU/RB/461832/2020**

115784802

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**KINGLION INVESTMENT COMPANY LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **KINGLION** yenye namba za usajili **MC 311 CBB.** Chassis **No.LTBPJ8BG2J2KO3401,** Engine No.**KLI57FMI18J03401..**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya polisi **DOD/DOD/RB/467330/2020.**

115784902

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**Evarist David Fumo** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba ya usajili **MC 825 ANW,** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi taarifa: **DAR/OST/RB/470841/2020**

115784202

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**MARIA LUCAS SANGOMA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 190 CHN SANLG.** YEYOTE ATAKAE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE NA MARIA LUCAS SANGOMA KWA SIMU NAMBA **0759283740 AU 0762528292. RB NAMBA SHY/RB/2019.**

115784002


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Wamalawi kurudia uchaguzi urais leo

**LILONGWE, Malawi**

WANANCHI wa Malawi leo wataamua nani atakuwa rais wao kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, wakati watakapopiga kura kwa mara ya pili, baada ya uchaguzi wa awali Mahakama ya Kikatiba kutupilia mbali matokeo yake.

Rais aliye madarakani, Peter Mutharika alitangazwa mshindi Mei, 2019 baada ya kupata ushindi mdogo wa asilimia 38.5 ya kura zote zilizokuwa zimepigwa.

Lakini viongozi wa upinzani walipinga matokeo hayo mahakamani wakidai kwamba uchaguzi huo ulikumbwa na udanganyifu.

Majaji walikubaliana nao na kutupilia mbali matokeo hayo Februari, mwaka huu na kuagiza marudio ya uchaguzi huo.

Kwa sasa upinzani umeungana na kutoa mgombea mmoja ambaye atakabiliana na Rais Mutharika, anayewania muhula wa pili madarakani.

Kwa miezi kadhaa sasa, raia wa Malawi wamekuwa katika mgogoro wa kisiasa ambao haujawahi kushuhudiwa katika historia ya nchi hiyo.

Ni zaidi ya mwaka sasa tangu mamilioni ya raia wa Malawi walipojitokeza katika uchaguzi wa ubunge na urais.

Lakini katika uchaguzi utakaofanyika leo, nchi hiyo imegawanyika vikali. Kumekuwa na maandamano ya kupinga serikali pamoja na kutokea kwa ghasia ambako kumetishia nchi hiyo kutumbukia katika mgogoro mkubwa zaidi.

Mwenyekiti wa tume ya uchaguzi nchini Malawi, pia amejiuzulu huku wanachama wapya wa tume hiyo wakichaguliwa ili kusimamia uchaguzi huo.

Uchaguzi huu ni kinyang'anyiro cha kati ya Mutharika dhidi ya mpinzani wake, Lazarus Chakwera, aliyekuwa mwinjilisti.

Chakwera ameunganisha upinzani chini ya muungano ambao unaonekana kuwa tayari kukabiliana na chama tawala cha Democratic Progressive ambacho kiliundwa 2004 na kaka yake rais wa sasa.

Uchaguzi huu pia unafanyika chini ya sheria tofauti baada ya mahakama kutoa uamuzi kwamba mfumo wa uchaguzi uliopita (anayepata kura nyingi hata kama hajafikisha asilimia hamsini ya kura zilizopigwa anatangazwa mshindi) ulikuwa kinyume na katiba.

Atakayeibuka na ushindi kati ya wagombea hao wawili, atakuwa na kibarua kigumu cha kukabiliana na mgawanyiko uliojitokeza na kumaliza ghasia ambazo zimekuwa zikishuhudiwa katika kipindi cha mwaka moja uliopita.

Pia atakuwa na kazi ya kukabiliana na ufisadi, kupunguza umaskini na ukosefu wa ajira ni miongoni mwa masuala ya msingi katika uchaguzi huo.

Raia wa Malawi wana imani kwamba sauti zao zitasikika na kuwa leo pengine huenda ikawa ndiyo mwanzo mpya kwa nchi hiyo.

***BBC***



Kiongozi wa chama cha upinzani nchini Malawi, Lazarus Chakwera, akiwa katika moja ya mkutano wa kampeni. **PICHA: REUTERS**

# Matajiri watakaoshindwa kujieleza kunyang'anywa mali

**HARARE, Zimbabwe**

MAMLAKA ya Zimbabwe imesema watu ambao hawawezi kuelezea namna utajiri wao ulivyopatikana, mali zao ziko katika hatari ya kuchukuliwa.

Mwenyekiti wa Tume ya Kupambana na Ufisadi Zimbabwe, Jaji Loyce Matanda-Moyo, alisema operesheni mpya nchini humo ni kuchunguza maisha ya matajiri.

Nchi hiyo inakabiliana na mdodoro wa kiuchumi katika kipindi cha mwongo mmoja sasa.

Raia wamekuwa na hasira juu ya huduma mbovu zinazotolewa, huku ufisadi ukiendelea kukithiri.

"Huu ni uchunguzi wa maisha ya baadhi ya watu matajiri. Watahitajika kutoa stakabadhi zao kuonyesha bidhaa na huduma wanazatoa na zitahitajika kuendana na thamani ya mali walizonazo. Pia tutaangalia ikiwa watu hawa au biashara zao walikuwa wanalipa ushuru," alisema Justice Matanda-Moyo.

Katika operesheni hiyo, tume hiyo inatumia madaraka iliyopata kuanzia Julai, 2019 ya kutaka kuelezewa namna watu walivyopata utajiri wao kulingana na kile kinachofahamika kama utajiri usioweza kuelezeka.

Watu wanaochunguzwa wanaweza kwenda katika mahakama ya juu kuelezea utajiri wao, lakini iwapo hawatafanya hivyo moja kwa moja mali zao zinachukuliwa.

Zimbabwe siyo nchi ya kwanza kuchukua hatua kama hiyo kutaka watu kuelezea vile walivyopata utajiri wao. Ireland na Uingereza zote zilibadilisha sheria zao na kuanzisha sheria ya mali isiyoweza kuelezeka kule ilikotoka 2017.

Shirika la Kimataifa la Kupambana na Ufisadi Transparency International, hivi karibuni lilitaja vifaa vya kimatibabu kukabiliana na virusi vya corona vilivyoagizwa na Zimbabwe kama wenye mashaka.

Shirika hilo lilisema kuwa bei za vifaa vya matibabu zilizongezwa na kuashiria uwezekano wa ufisadi unaoendelea nchini humo.

Aidha, Jumamosi, Waziri wa Afya, Obadiah Moyo alishtakiwa kwa makosa ya kutumia vibaya mamlaka yake yenye kuhusishwa na kandarasi ya uagizaji wa bidhaa hizo.

***BBC***

## Rais Kenyatta, William Ruto waendelea kutofautiana

**NAIROBI, Kenya**

UHUSIANO wa siasa kati ya Rais Uhuru Kenyatta na Makamu wake, William Ruto, umeendelea kusambaratika zaidi baada ya mshirika muhimu na wa karibu wa Ruto, Aden Duale kuondolewa kwenye kiti cha kiongozi wa wengi katika bunge la taifa.

Uamuzi wa kutimuliwa kwa Duale uliamuliwa na chama tawala nchini humo cha Jubilee na nafasi yake ikichukuliwa na mbunge Kipipiri Amos Kimunya.

Duale alikuwa kwenye wadhifa huo tangu chama cha Jubilee kipate ushindi mwaka 2013.

Mabadiliko hayo yanajiri wakati Rais Kenyatta akijitahidi kujenga uaminifu wake katika muhula wake wa pili na wa mwisho.

Rais Kenyatta alinukuliwa akisema kuwa anaondoa viongozi ambao wanaonekana kuwa vizuizi katika ajenda zake.

Mkutano wa chama hicho uliodumu kwa kipindi cha dakika 25, ulikuwa na agenda moja tu, kumng'oa Duale.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa kwenye mkutano huo makamu Ruto alihudhuria japo hakupewa nafasi ya kuzugumza. Alitulia na kutazama maamuzi yalipokuwa yakifanyika.

Wabunge 150 wa chama hicho walihudhuria mkutano huo, japo baadhi walituma ombi la kutokuhudhuria.

Hatua ya Ruto ya kufungua ofisi sanjari ya chama tawala kwa jina Jubilee Asili wiki iliyopita huenda ilimkasirisha Rais Kenyatta.

Hata hivyo, suala hilo halikujadiliwa kwenye mkutano huo.

Katika mkutano wa chama hicho uliofanyika mwanzoni mwa mwezi huu, Amos Kimunya alipewa nafasi ya kuwa katibu wa mikutano yote ya chama hicho.

Mnadhimu mkuu wa chama hicho, Benjamin Washiali, na makamu wake, Cecily Mbarire, waliondolewa pia kwenye viti vyao.

Seneta Kipchumba Murkomen, aliyekuwa kiongozi wa wengi katika Baraza la Seneti pamoja na makamu wa spika katika baraza hilo, Kithure Kindiki, walishaondolewa kwenye viti vyao kwa kile kilichosemekana kukosa uaminifu kwa chama. Wote walikuwa washirika wa karibu wa siasa wa Ruto.

Chama kipya kinachohusishwa na Ruto cha Jubilee Asili hakijazinduliwa rasmi, lakini kinajumuisha wajumbe wote walioondolewa kwenye viti vya kamati za bunge.

**DW**



# ERIKSEN

## AFUNGUKA KUHUSU KIWANGO CHAKE

**MILAN, Italia**

CHRISTIAN Eriksen amesema hajafikia ubora wake tangu ajiunge na Inter Milan, lakini anaangalia namna ya kujiimarisha zaidi baada ya kuonyesha kiwango cha kuvutia wakati wakishinda mabao 2-1 dhidi ya Sampdoria kwenye mchezo wa Ligi Kuu Italia, juzi.

Eriksen alikuwa kwenye kiwango chake kwenye mchezo huo wa Jumapili akitengeneza bao la kwanza la Inter wakati ligi hiyo iliporudi tena.

Nyota huyo wa zamani wa Tottenham Hotspur amekuwa na wakati mgumu tangu alipoondoka kwenye Ligi Kuu England na kujiunga na Inter Januari, lakini sasa Eriksen ameonekana kuwa bora tangu kurejea kwa ligi hiyo baada ya mlipuko wa virusi vya corona.

Eriksen alimtengenezea Romelu Lukaku bao katika dakika ya 10 kabla ya Lautaro Martinez kufunga la pili dakika ya 23 kwenye mchezo uliopigwa katika dimba la San Siro.

Baada ya mchezo huo raia huyo wa Denmark aliiambia Sky Sport: "Sidhani kama mmemwona Eriksen wa ukweli.

"Naweza kuimarika zaidi na nina matumaini ya kufunga zaidi, nilifanya hivyo dhidi ya Napoli, lakini sikuweza kuisaidia timu.

"Lakini sasa naweza kusema ubora wangu unakuja na nitakuwa kwenye kiwango cha kuvutia, na nataka kuwa katika ubora wangu."

## CARRAGHER: ARSENAL HAWAKO VIZURI

**LONDON, England**

MLINZI wa zamani wa Liverpool, Jamie Carragher amesema kocha wa Arsenal, Mikel Arteta ana kazi kubwa ya kufanya, ili kukiwezesha kikosi chake kuwa na makali kwa siku za usoni.

Carragher, ambaye kwa sasa ni mchambuzi wa soka, amesema kikosi cha Arsenal hakiko vizuri na kilionekana dhaifu wakati kikipambana na Manchester City, huku akionya kuwa Arteta anahitaji kufanya kazi kubwa kukibadili kikosi hicho.

Mchezo huo ulikuwa wa kwanza kwa Arsenal kwenye Ligi Kuu England iliyosimama kwa miezi miwili kutokana na kusambaa kwa virusi vya corona, lakini wakaruhusu idadi kubwa ya mabao wakiwa kwenye Uwanja wa Etihad.

"Sikutarajia kuona kitu tofauti na kile nilichokiona kwenye mchezo ule. Nilichokiona ambacho Arsenal wamekifanya ndio kinachotokea kwa karibu misimu 10 sasa, hakukuwa na tofauti kubwa," alisema beki huyo aliyeshinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Liverpool.

Katika mchezo huo, Arsenal walianza kupotea mapema kabla ya kipindi cha kwanza baada ya beki wake David Luiz kufanya kosa la kizembe na kumpa nafasi Raheem Sterling kupachika bao la kwanza.

Mbrazili huyo aliyeingia kuchukua nafasi ya Pablo Mari aliyeumia mapema tu, alizamisha jahazi la Arsenal kwa mara nyingine baada ya kumfanyia madhambi winga wa City, Riyad Mahrez ndani ya eneo la hatari na mwamuzi kuamuru penalti iliyozamishwa wavuni na Kevin De Bruyne.

Mbali na City kuzawadiwa penalti, Luiz alilimwa kadi nyekundu na kuifanya Arsenal kucheza ikiwa pungufu na kinda, Phil Foden kufunga bao la tatu.

Kutokana na hilo, Caragher alisema kuwa: "Arsenal hawako vizuri. Sioni dalili kama wanaweza kuingia ndani ya 'Top Four' kwani, wana tofauti kubwa ya pointi."

# RAMOS

## AWEKA REKODI YA UFUNGAJI LALIGA

**MADRID, Hispania**

NAHODHA wa Real Madrid, Sergio Ramos amekuwa mlinzi wa kwanza kufunga mabao mengi zaidi katika historia ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, baada ya kufunga bao Jumapili.

Ramos alifikisha mabao 68 baada ya kufunga kwa mkwaju wa penalti wakati Madrid wakikwea kileleni mwa msimamo wa LaLiga baada ya ushindi wa magoli 2-1 dhidi ya Real Sociedad.

Ramos alifunga bao hilo kwa kumpeleka maboya golikipa Alex Remiro baada ya Vinicius Junior kufanyiwa madhambi eneo la hatari.

Ramos aliifuta rekodi ya mlinzi wa zamani wa Barcelona, Ronald Koeman kwa kuwa mfungaji wa wakati wote kwa upande wa mabeki.

Ramos mwenye umri wa miaka 34 pia alifanya kazi ya ziada wakati Karim Benzema akifunga bao la pili kwa Madrid dakika 10 baadaye.

Ramos, ambaye alikulia katika klabu ya Sevilla alijiunga na Real Madrid mwaka 2005 na ameshinda mataji 21 yakiwamo manne ya LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

# SPURS YAPIGIA HESABU LIGI YA MABINGWA ULAYA

**LONDON, England**

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho amesisitiza timu yake inahitaji kufanya vizuri katika michezo tisa mfululizo iliyobakia ya Ligi Kuu England, ukiwamo dhidi ya Manchester United utakaochezwa leo ili kuhakikisha wanapata nafasi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Spurs ambao wapo nafasi ya nane katika msimamo wa Ligi Kuu England wakiwa na pointi 41, kabla ya kusitishwa kwa ligi hiyo kutokana na janga la virusi vya corona, ilitwaa pointi 16 kati ya 27, wakiwa chini ya Mourinho ambaye amerithi mikoba ya Mauricio Pochettino. "Kwa sasa tunahitaji zaidi ya hiyo idadi ya michezo kwa sababu tumepoteza pointi nyingi na kujiweka katika nafasi ngumu.

Ni vita ngumu. Sidhani kama tunaweza kupoteza alama nyingi, isipokuwa wapinzani wetu wa moja kwa moja au watano wapoteze alama nyingi," alisema Mourinho.

Spurs haikuwa katika kiwango bora cha ushindani kutokana na sehemu kubwa ya wachezaji wao wa kikosi cha kwanza kuandamwa na majeruhi, ambao sasa wamepona, na Mourinho anaamini wataongeza nguvu katika kikosi chake.

"Ilikuwa ni nafasi ya kuwa karibu na kila mmoja wetu kama timu na kuwa kitu kimoja, ulikuwa ni wakati mzuri mno.

"Wachezaji naamini walifurahia kuwa pamoja kwa sababu ulikuwa ni wakati mgumu hivyo tulipenda kuwaweka karibu na viongozi ili kujenga kitu ndani yao, tuliondoa simanzi ya marufuku ambayo ilikuwapo," alisema Mourinho.

# UNITED, LIVERPOOL ZAMGOMBEA JIMENEZ

**MADRID, Hispania**

REAL Madrid, Manchester United na Liverpool zinaonyeshana shughuli kuwania saini ya mshambuliaji matata wa Wolves, Raul Jimenez.

Nyota huyo wa Mexico, Jeminez amekuwa kwenye kiwango bora kwa misimu miwili sasa na kuiweka Wolves kwenye daraja la juu, na sasa amefunguka kuwa yupo tayari kukipiga kwenye moja kati ya Real Madrid, Manchester United na Liverpool.

Msimu huu amefunga mabao 22 kwenye mechi 44 za michuano yote na hilo limewafanya wababe hao kuanza kuweka rada ili kuboresha safu za ushambuliaji ambazo zote zinahitaji watu wapya.

Habari kutoka kwenye korido za Wolves zinasema kwamba, klabu nyingi zimeonyesha nia ya kutuma ofa kwa ajili ya Jeminez pindi dirisha la usajili litakapofunguliwa.

Hata hivyo, Jimenez mwenyewe amekiri kwamba, hatua ya wababe hao kuonyesha dhamira ya kutaka huduma yake itampa mzuka wa kufanya vizuri zaidi uwanjani.


"Ni kitu kizuri sana kama ni kweli wanavutiwa na huduma yangu," alisema Jimenez wakati wa mahojiano na Jesca Coch.

"Klabu kama Real Madrid, Barcelona, Juventus, Manchester City, Manchester United na Liverpool zina historia kubwa kwenye soka na uwepo wao una maana kubwa sana.

"Ni jambo la kuvutia kuwapo kwenye rada zao kama mchezaji, ni jambo zuri kwangu kwani itanifanya niongeze bidii uwanjani. Kucheza kwenye klabu hizi inabidi uwe na ubora mkubwa. Kama itawezekana basi tusubiri," alisema Jimenez.

Hata hivyo, alipoulizwa na klabu gani anatamani kwenda kuichezea kati ya hizo tatu, alisema: "Timu ya ndoto yangu? Yoyote kati ya hizo itakuwa nzuri kwangu, japo siwezi kusema moja wapo hadharani."

Wolves inayosaka nafasi ya kumaliza ndani ya nafasi nne za juu ili kupata nafasi ya kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao, itakuwa na West Ham United kesho.



# LIVERPOOL YAMWANIA MBAPPE

**LIVERPOOL, England**

LIVERPOOL inafikiria kumsajili, Kylian Mbappe anayewaniwa pia na Real Madrid kwa hofu juu ya majaliwa ya Sadio Mane hapo kwenye dimba la Anfield, kwa mujibu wa gazeti la The Sun.

Kwa muda mrefu sasa, Real Madrid imekuwa ikitajwa kutaka kumsajili Mbappe ambaye amekuwa kwenye kiwango kizuri kule Paris Saint-Germain.


Inafahamika wazi kuwa Kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane anavutiwa sana na nyota huyo wa PSG ambaye ni mshindi wa Kombe la Dunia mwaka jana.

Lakini Jurgen Klopp anataka kuongeza nguvu kwenye kikosi chake cha Liverpool hasa kutokana na uvumi anaweza kumkosa Mane wakati dirisha la usajili la majira ya joto litakapofunguliwa.

Mane mkataba wake na Liverpool unamalizika mwaka 2023, lakini kuna tetesi kwamba, Msenegali huyo anawaniwa sana na Madrid pamoja na Paris Saint-Germain.

Hivyo, Liverpool wanafikiria kumsajili Mbappe ili awe mbadala wa Mane na wameripotiwa wapo tayari kutoa kiasi cha pauni milioni 200.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# BARCA, MESSI WAFIKIA PAZURI

Kuhusiana na mazungumzo ya kusaini mkataba mpya ambao utamweka nyota huyo Katalunya hadi...

**BARCELONA, Hispania**

MAZUNGUMZO ya kusaini mkataba mpya kati ya Lionel Messi na Barcelona 'yanaendelea vizuri', taarifa mbalimbali zimeripoti.

Klabu hiyo ya Katalunya na nyota huyo wa Timu ya Taifa ya Argentina wamefikia makubaliano ya kusaini mkataba mpya, lakini kila upande umeeleza wamekaribia kukamilisha mchakato huo wa kusaini mkataba wa miaka miwili.

Kwa mujibu wa gazeti la Marca la Hispania, limeandika makubaliano kuhusu muda wa mkataba huo mpya na kiasi cha mshahara atakacholipwa Messi kitafikiwa ifikapo majira ya joto.

Mazungumzo hayo yanafanyika kati ya Rais wa Barca, Josep Maria Bartomeu na Jorge Messi, ambaye ni baba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32.

Klabu hiyo ya LaLiga inaamini Messi atakubali kuongeza mkataba mpya ambao utakuwa wa miaka miwili, utakaomfanya nyota huyo akae Katalunya hadi mwaka 2023.

Hata hivyo, katika mkataba wake unaomalizika, kuna kipengele kinachoruhusu mshambuliaji huyo kuondoka klabuni hapo kila baada ya msimu kumalizika.

Hii inaonekana kuwa Messi hataki kujibana kwenye mkataba wake.

Mshindi huyo wa tuzo ya Ballon d'Or ataendelea kulipwa mshahara wa pauni 500,000 kwa wiki licha ya kuwapo kwa mtikisiko wa kiuchumi uliosababishwa na janga la corona.

Barca pia inatajwa kuanza tena mazungumzo na golikipa wake, Marc-Andre ter Stegen baada ya majadiliano ya awali kuwekwa kiporo kutokana na mapumziko ya mchezo huo yaliyotokana na corona.

Lakini klabu hiyo kongwe ya Hispania imejipanga kurejesha tena mazungumzo pamoja na Mjerumani huyo.

## KWA UFUPI

**GUARDIOLA AFUNGUKA**
KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amekiri hatatafuta mbadala wa Leroy Sane endapo nyota huyo ataondoka, lakini atajiandaa kuimarisha safu yake ya ulinzi kuelekea msimu mpya. ***(Standard)***

**CHELSEA YAMTAJA KURZAWA**
CHELSEA itarejea katika mchakato wa kuwania saini ya beki wa kushoto wa Paris St-Germain na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Layvin Kurzawa (27), kama itashindwa kunasa saini ya nyota wa Leicester na England, Ben Chilwell (23). ***(Express)***

**JIMINEZ AKARIBIA JUVE**
JUVENTUS iko tayari kuwatoa wachezaji wake Wataliano beki, Daniele Rugani (25), na winga Federico Bernardeschi (26), kwa Wolves ili kurahisisha dau la kumpata straika wa Timu ya Taifa ya Mexico, Raul Jimenez (29). ***(Tuttosport)***

**LIVER YAMTAKA KOULIBALY**
LIVERPOOL imewasilisha ofa ya pauni milioni 54 ili kumsajili beki wa Napoli na Timu ya Taifa ya Senegal, Kalidou Koulibaly. Beki huyo mwenye umri wa miaka 29 pia anawindwa na Chelsea na Manchester United. ***(Corriere dello Sport)***

**ROMA YAMFUATA VERTONGHEN**
ROMA imempa ofa ya mkataba wa miaka miwili beki wa Tottenham na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Jan Vertonghen (33), ambao pia utakuwa wa kipengele cha kusaini mkataba mwingine wa kuitumikia timu hiyo kwa msimu wa tatu. ***(Il Messaggero, via Mail)***

**SALISU ATAKIWA EVERTON**
EVERTON imeingia kwenye mbio za kuwania saini ya beki wa Real Valladolid, Mohammed Salisu (21). Mghana huyo ambaye thamani yake imetajwa kuwa ni pauni milioni 10.8, pia anawindwa na Southampton na Manchester United. ***(Mail)***

**MORGAN KUTUA NICE**
KIUNGO wa Everton na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Morgan Schneiderlin (30), anajiandaa kuondoka Goodison Park baada ya kufaulu vipimo vya afya katika klabu ya Ligue 1 ya Ufaransa ya Nice. ***(Sky Sports)***

**CITY YAMNASA KRASTEV**
MABOSI wa PFC Slavia Sofia wamesema tayari wameshafikia makubaliano na Manchester City kwa ajili ya kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Bulgaria, Filip Krastev (18). ***(Manchester Evening News)***

**CARROLL KUBAKIA NEWCASTLE**
STRAIKA wa Newcastle, Andy Carroll, ambaye ana umri wa miaka 31, atabakia St James' Park kwa msimu mwingine baada ya kusaini mkataba mwingine ambao unamweka tena klabuni hapo. ***(Sunday Mirror)***

**SANCHEZ AITWA VALLADOLID**
RAIS wa Real Valladolid, Ronaldo Nazario amefungua milango kwa Alexis Sanchez kujiunga na timu hiyo. Winga huyo wa Timu ya Taifa ya Chile yuko kwa mkopo katika klabu ya Inter Milan akitokea Manchester United.

**BELLINGHAM APEWA HESHIMA**
MAOFISA wa Birmingham City wamemwandalia kiti maalumu mama wa mchezaji wake, Jude Bellingham kwa ajili ya kuangalia mechi ya Ligi ya Championship katika mechi dhidi ya West Brom. Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 16, anatakiwa na Manchester United na Borussia Dortmund. ***(Mail)***

## HABARI MICHEZO

# NAMUNGO YAIZIDI 'KETE' YANGA KUMSAJILI LUSAJO

**Na Saada Akida**

UNAWEZA kusema Yanga 'imekula kwao' baada ya uongozi wa Namungo FC kuwa kwenye nafasi nzuri ya kumbakisha mshambuliaji wake, Reliants Lusajo katika kikosi hicho kwa ajili ya msimu ujao, imefahamika.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Meneja wa mchezaji huyo, Ahmad Omary 'Prezidaa' alisema mshambuliaji huyo yuko katika hatua nzuri za mazungumzo na klabu yake ambayo inashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

Prezidaa alisema Namungo inataka kumpa Lusajo mkataba mpya wa kuendelea kutumikia timu hiyo kabla ya msimu huu haujamalizika.

Alisema wanatarajia kukutana na Mwenyekiti wa Namungo, Hassan Zidadu kwa ajili ya kukamilisha mazungumzo yao ambayo yatafuta ndoto za kujiunga na Yanga, ambayo pia ilionyesha nia ya kuhitaji huduma ya mshambuliaji huyo.

"Natarajia kukutana na mwenyekiti (Zidadu), nikiwa na mteja (Lusajo), wangu kuendelea na mazungumzo, kila mmoja wetu aweke mapendekezo mezani na kama yataenda sawa basi tutamalizana na kuongeza mkataba," alisema Prezidaa.

Aliongeza mpaka sasa anafahamu Namungo imedhamiria kumbakiza mshambuliaji huyo, lakini amefungua milango kwa timu zingine ambazo zinania ya kumsajili Lusajo.

Zidadu alisema kwa sasa wanapambana kuhakikisha wanawabakiza wachezaji wao wazuri walioisaidia timu hiyo ambao mikataba yao imemalizika akiwamo Lusajo.

"Tunafahamu kuna timu zinawahitaji baadhi ya wachezaji wetu, ndio maana tunaendelea kuzungumza nao kwa ajili ya makubaliano ya kuwabakisha," alisema Zidadu.

Alieleza wameshakutana na benchi la ufundi linaloongozwa na Mrundi Thiery Hitimana na kupokea mapendekezo ya nyota wanaowahitaji kuendelea nao ambao aliwataja baadhi ni Lusajo na Blaise Bigirimana.

Tayari kikosi cha Namungo kiko jijini tangu juzi kwa ajili ya kuwakabili Yanga katika mchezo wa Ligi Kuu Bara utakaochezwa kesho.



Wachezaji wa JKT Stars (wanawake), wakifanya mazoezi kujiandaa na mashindano mbalimbali yajayo ya mpira kwenye Uwanja wa Ndani wa Taifa jijini, Dar es Salaam juzi. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# Azam yaifuata Kagera Kaitaba

**Na Saada Akida**

WAKATI Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, amesema viungo wao hawakuwa bora na kuzidiwa katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Yanga iliyochezwa juzi, kikosi chake kimeondoka kuwafuata Kagera Sugar mkoani Kagera.

Azam ililazimisha suluhu na Yanga, na kuendelea kukoleza ushindani wa kuwania nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu Bara.

Vivier alisema mchezo huo ulikuwa mzuri kwa pande zote mbili, na wachezaji wao walijituma lakini walishindwa kutumia vema nafasi nyingi walizozitengeneza.

"Haikuwa siku yetu na ndio mpira jinsi ulivyo, kikubwa tunamshkuru Mungu kwa yote, kiungo cha Yanga kilikuwa imara huku tulimnyima nafasi, Haruna Ninyonzima maana alikuwa yupo vizuri, tungempa nafasi ya kutembea basi yule jezi namba 7, (Balama Mapinduzi) alikuwa hatari," alisema Vivier.

Aliongeza kukosekana kwa Frank Domayo na Salum Abubakar 'Sureboy" katika kikosi chao kilionyesha mapungufu na sasa wanayafanyia kazi ili kupata matokeo mazuri katika mchezo ujao.

"Bado hatujatoka katika malengo yetu ya kupambana katika nafasi ya pili, tunaenda ugenini kucheza na Kagera kutafuta ushindi," alisema kocha huyo.

Kagera Sugar inatarajia kuikaribisha Azam FC katika mchezo wa Ligi Kuu Bara utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.

## Mbao FC, Coastal Union hapatoshi

**Na Shufaa Lyimo**

LIGI Kuu Tanzania Bara inatarajia kuendelea leo katika viwanja vinne tofauti hapa nchini, huku Mbao FC ikiwakaribisha Coastal Union kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza.

Mbao FC inahitaji ushindi ili kujinasua kwenye janga la kushuka daraja wakati Coastal Union inataka kujiimarisha katika kufikia malengo yake ya kumaliza katika nafasi tano za juu.

Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda, aliliambia gazeti hili anatarajia mechi hiyo itakuwa na ushindani kwa sababu wenyeji wao wako katika nafasi mbaya.

Mgunda alisema anafahamu Mbao itahitaji kutumia vema uwanja wake wa nyumbani, lakini naye anahitaji kuendelea kuvuna pointi bila kujali anacheza kwenye uwanja wa ugenini.

"Hakuna mechi rahisi, dakika hizi za lala salama, kila mtu anataka kujiimarisha, tumejipanga na tunaamini tutapata chochote kama tutatulia na kufanya kile tulichokiandaa," Mgunda alisema.

Mechi nyingine za ligi hiyo zitakazochezwa leo ni Tanzania Prisons dhidi ya JKT Tanzania wakati Ruvu Shooting itawakabili Ndanda FC, Singida United itawavaa Mtibwa Sugar na Lipuli FC imewafuata Mwadui FC.

## Ligi Kuu Zanzibar yapigwa kalenda

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

LIGI Kuu Zanzibar sasa itaanza kuchezwa ifikapo Julai Mosi, mwaka huu badala ya kesho kama ilivyokuwa imetangazwa hapo awali, imefahamika.

Uamuzi huo umetolewa baada ya Wizara ya Michezo kukutana na Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), ili kujadili maombi ya baadhi ya timu zilizohitaji ligi hiyo kuchezwa katika vituo viwili kama ilivyokuwa hapo nyuma.


Timu zimeomba mechi zichezwe katika mtindo wa nyumbani na ugenini ili kupunguza gharama za kuchezwa kwenye kituo kimoja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaimu Katibu wa ZFF, Ali Ame Vuai, alisema shirikisho hilo kwa kushirikiana na wizara husika lipo katika mchakato wa kuona maombi ya vilabu hivyo yanafanyiwa kazi kwa kadri itakavyowezekana.

Vuai alisema serikali iliamua ligi hiyo kuchezwa katika kituo kimoja kulingana na taratibu za kiafya zilizotolewa kwenye kipindi hiki cha mapambano dhidi ya corona.

"ZFF itasubiri uamuzi mwingine utakaotolewa na serikali baada ya kuangalia uwezekano wa ligi kuchezwa katika vituo viwili wakati huu wa corona," Vuai alisema.

Michezo
Jumanne Juni 23, 2020
Nipashe



## Barca, Messi wafikia pazuri

HABARI UK 22



Mshambuliaji wa Yanga, Yikpe Gislain (kushoto), akiwania mpira dhidi ya beki wa Azam FC, Oscar Masai katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam juzi. Timu hizo zilitoka suluhu. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# YANGA YAWEKA REKODI LIGI KUU

●●●Kikosi hicho cha Mbelgiji Eymael kinaongoza kwa kutoa sare, huku kila timu ikiwa imebakisha mechi nane kumaliza...

**Na Adam Fungamwango**

SULUHU iliyopata dhidi ya Azam FC kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam Jumapili jioni, imeifanya Yanga kuingia kwenye rekodi ya kutoka sare nyingi zaidi msimu huu tangu kuanza kwa mfumo mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Yanga, ambayo ilitoka sare ya bila kufungana dhidi ya Azam imeifanya timu hiyo kufikisha sare 11 msimu huu, hali ambayo haijawahi kuipata kabla, tangu msimu wa 2007/08 ambao ulikuwa ni msimu wa mfumo mpya wa Ligi Kuu Tanzania, ikianzia Agosti au Septemba badala ya Januari au Februari kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Timu hiyo imebakisha mechi nane, hivyo inaweza kabisa idadi ya sare kuongezeka kabla ya kumalizika kwa msimu huu wa mwaka 2019/20.

Kwa mujibu wa rekodi, ni kwamba mara ya mwisho Yanga kupata sare nyingi kwenye Ligi Kuu Bara ilikuwa ni msimu wa 2017/18 ilipotoka sare mara 10, ikikamata nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi, Simba ikitwaa ubingwa na Azam ikichukua nafasi ya pili.

Rekodi zinaonyesha msimu wa 2007/08 Yanga ilitoa sare saba ikiwa bingwa na msimu uliofuata 2008/09 ilitwaa ubingwa pia, ikiwa imetoa sare tatu tu.

Msimu wa 2009/10, Yanga ilitoa sare mara nne, ikikamata nafasi ya pili nyuma ya Simba ilikuwa bingwa na msimu wa 2010/11 ilitoka sare mara saba.

Msimu wa 2011/12, Yanga ilikamata nafasi ya tatu kwenye Ligi Kuu Bara, lakini ikiwa imetoa sare nne tu, Simba ikiwa bingwa na Azam kushika nafasi ya pili na msimu wa 2012/13, ilitwaa ubingwa ikiwa imemaliza ligi ikitoa sare sita.

Msimu wa 2013/14 ambao Azam ilifanikiwa kutwaa ubingwa kwa mara ya kwanza, Yanga ilikamata nafasi ya pili, ikiwa imetoka sare mara nane na msimu uliofuata 2014/15, ilitwaa ubingwa ikiwa imepata sare nne tu.

Yanga ilifanikiwa kupata sare saba msimu wa 2015/16 ikitwaa tena ubingwa na msimu uliofuata 2016/17, ilitwaa tena ubingwa ikiwa imepata sare tano.

Simba ilitwaa ubingwa msimu wa 2017/18, Azam ikishika nafasi ya pili, Yanga ikiwa ya tatu na sare zake 10, huku msimu uliopita wa 2018/19, Yanga ikishika nafasi ya pili nyuma ya Simba, lakini ikiwa imetoka sare mara tano tu.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Bara inayotarajiwa kuendelea tena leo, Yanga iko katika nafasi ya tatu ikiwa na pointi 56 wakati Azam FC yenye pointi 57 iko juu yake, huku mabingwa watetezi, Simba wakiwa kileleni na pointi zao 75.

Ligi hiyo ndio inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, huku michuano ya Kombe la FA ambayo iko kwenye hatua ya robo fainali kuipa bingwa tiketi ya kupeperusha bendera ya nchi katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

## HATIMA NYOTA WAGENI YANUKIA

**Na Somoe Ng'itu**

SERIKALI imesema itatoa mwongozo kuhusu wachezaji wa kigeni watakaoruhusiwa kusajiliwa na timu zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara hivi karibuni, imeelezwa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, alisema ni lazima uandaliwe utaratibu wa kuruhusu wachezaji hao wa kigeni ambao unalenga zaidi kukuza vipaji vya nyota wazawa.

Mwakyembe alisema serikali haitakubali kuona wachezaji wasiokuwa na viwango wanasajiliwa na klabu za hapa nchini kwa sababu uamuzi huo unawanyima nafasi wachezaji Watanzania ambao wanaibukia.

"Ukiruhusu kila mchezaji aje, hatutakuza vipaji vya vijana wetu wanaochipukia kila mwaka, tutatoa uamuzi hivi karibuni, sisi ndio tunaotoa vibali, lazima tuwe na vigezo, sio tukubali tu, tutajadiliana ili kufikia uamuzi utakaokuwa na faida kwetu," alisema Mwakyembe.

Waziri huyo pia amezishauri Simba na Yanga kufanya tathmini mpya ili kupata thamani halisi za klabu hizo kongwe hapa nchini.

Alisema haamini kama Simba ina thamani ya Sh. bilioni 20, na kuelekeza klabu hizo kutumia kampuni za kimataifa ili kutekeleza mchakato huo huku zikiendelea na taratibu za kubadili mfumo wa uendeshwaji.

## SIMBA YAWASILI MBEYA KIBABE

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba kiliwasili salama Mbeya jana asubuhi tayari kwa mechi yao dhidi ya wenyeji Mbeya City, itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Sokoine jijini humo.

Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema kikosi hicho kimesafiri na wachezaji 26, na wamekwenda mkoani humo kwa kazi moja ya kuendelea 'kuvuna' pointi.

"Tunajua mchezo huu unasubiriwa na mashabiki kwa shauku kubwa, hii inatokana na endapo tutashinda, tutakuwa tunajiweka kwenye harufu ya ubingwa mapema," alisema Rweyemamu. Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, aliwataka wachezaji wake kuendelea kujituma na kuongeza umakini kila watakavyotengeneza nafasi za kufunga na kuwataka wacheze kwa tahadhari.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >